**ACT** - Wazalendo yazinyooshea kidole shida kuu 5 kwa wananchi

UKURASA 3



**Waangua** kilio kwa Chongolo kisa mradi maji

UKURASA 3


ama

AFYA NA MAZINGIRA

RC ashika bango dai la ushoga mkoani, vikao madiwani kashfa zawasha moto

Mwakilishi UNFPA: Kinga vito vya wajawazito, 'vichanga' ni wakunga

Waziri Tamisemi Mchengerwa 'mikataba' ... Ulanga, ... Rais Samia

- Ujuzi kutika kila mkoa; ubia na Zambia, Rwanda...

UKURASA 11


# Nipashe

Alhamisi Juni 1, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581328

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


# Kwaheri giza



Mashine kuwashwa Bwawa la Nyerere

Hifadhi ya mafuta yaundiwa mkakati

Kila kijiji sasa kupelekewa umeme

Gesi, majiko ya kisasa kusambazwa vijijini

*Endelea ukurasa 2*

# Serikali yataja sababu vichwa vya treni SGR kutofika nchini

UKURASA 8



# Dk. Mwinyi azindua Kamati ya Maridhiano kumaliza uhasama

UKURASA 2






Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na viongozi wa vyama vya CCM na ACT-Wazalendo, alipozindua Kamati ya Maridhiano ya vyama hivyo, Ikulu jijini Zanzibar jana. Kulia kwa Rais ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla na (kushoto kwa Rais) ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman. **PICHA: IKULU**

# Kwaheri enzi za giza

**Na Waandishi Wetu, D**ODOMA

KWAHERI giza! Ndicho unachoweza kusema kutokana na mikakati ya Wizara ya Nishati kwa mwaka ujao wa fedha kujikita katika upatikanaji umeme.

Kwa mwaka huo wa fedha, nchi itaingia katika historia kwa kuwasha mashine ya kwanza katika Mradi wa Kufua Umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere na umeme wake kuingiza umeme gridi ya taifa.

Ni mikakati iliyowakosha wabunge wengi kiasi cha baadhi yao kutaka kusiwe na mjadala kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha bali yapitishwe tu. Waendelee na majukumu mengine.

Wizara imejikita katika matumizi ya nishati mbadala, uchumi wa gesi na nchi kuongeza uwezo wa kuwa na akiba kubwa zaidi ya mafuta.

Akiwasilisha makadirio hayo bungeni jijini hapa jana, Waziri January Makamba aliliomba Bunge kuidhinisha Sh. trilioni 3.05 kwa ajili ya utekelezaji. Kati yake, Sh. trilioni 2.9 (asilimia 97.1) ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo - Sh. trilioni 2.6 ni fedha za ndani na Sh. bilioni 351.5 ni fedha za nje.

January alibainisha kuwa hadi kufikia Juni mwakani, vijiji 12,318 vitafikiwa na umeme, pia ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme katika vitongoji 2,034, kilometa 4,246 za msongo mdogo zinakwenda kujengwa na mikoa tisa kunufaika na ufungaji wa mashine umba 1,277 na kuunganisha wateja wa awali 95,334.

Pia majiko banifu 70,000 yatasambazwa vijijini na vijiji-miji na mitungi 200,000 kutolewa kwa wananchi pamoja na mifumo ya kupikia kwa gesi asilia katika taasisi mbalimbali.

### JNHPP

Waziri huyo alisema katika kipindi cha wiki moja kuanzia jana, bwawa la Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Maji wa Julius Nyeree (JNHPP) litafikisha kiwango cha ujazo wa maji (yaani mita 163 kutoka usawa wa bahari) kinachowezesha kuanza uzalishaji wa umeme.

"Kiwango cha chini ni mita 163 kutoa usawa wa bahari na tumebakiza mita kama mbili kufikia kiwango hicho na tutafika huko. Katika mwaka ujao wa fedha, tutakamilisha ufungaji wa mitambo ya kuzalisha umeme; kujenga njia ya kusafirisha umeme kutoka katika kituo cha kufua umeme hadi kituo cha kupokelea umeme.

"Pia tutakamilisha barabara ya kudumu katika eneo la mradi. Katika mwaka ujao wa fedha tutafanya tukio lingine la kihistoria la kuingiza umeme wa Julius Nyerere kwenye gridi ya taifa kwa mara ya kwanza," alisema.

Waziri huyo alisema serikali kupitia TANESCO itaanza utekelezaji wa miradi ya kijamii (CSR) inayotokana na makubaliano ya mkataba wa ujenzi wa JNHPP na kwa kuanzia itajenga chuo kikubwa cha kisasa cha ufundi wa umeme na mafuta na gesi mkoani Lindi na utakamilika mwezi Juni mwakani.

Alisema serikali pia itaanza maandalizi ya mradi wa kusindika gesi wa LNG mkoani Lindi na kumalizia kazi ya kupeleka umeme katika vijiji vyote vilivyopo nchini.

### MADENI TANESCO, TPDC

January alisema serikali iliridhia mapendekezo ya kubadili madeni makubwa yaliyokuwa yanayakabili mashirika ya TANESCO na TPDC, ili kuyafanya yawe na rekodi nzuri katika vitabu vyake vya hesabu. "Serikali ilibadili madeni ya TANESCO yanayofikia Sh. trilioni 2.4 kuwa mtaji wa shirika. Pia ilibadili mkopo wa mradi wa ujenzi wa bomba na mitambo ya kuchakata gesi asilia wa dola za Marekani bilioni 1.19 kuwa mtaji wa serikali kwa TPDC. Hatua hii itaimarisha mizania ya hesabu za mashirika hayo," alisema.

Kuhusu matumizi ya nishati mbadala alisema, kwa mara ya kwanza Tanzania itaingiza megawati 50 za umeme wa jua katika gridi ya taifa katika mwaka ujao wa fedha.

Alisema upatikanaji umeme kwa sasa jumla ya vijiji vilivyounganishwa na umeme nchini vimefikia 10,127 sawa na asilimia 82 ya vijiji vyote 12,318 na lengo ni kuhakikisha umeme unafika kwenye vijiji vyote.

Alisema serikali itaendelea na miradi ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya kimkakati na imetenga Sh. bilioni 12.6 kwa ajili ya usambazaji katika maeneo ya viwanda, majumbani na taasisi.

### HIFADHI MAFUTA

Waziri January alisema wanakwenda kujenga miundombinu ya hifadhi ya mikakati ya mafuta pamoja na miundombinu ya kuwezesha biashara ya mafuta. Watakamilisha taratibu za kumpata mkandarasi kwa ajili ya ukarabati wa tangi Na. 8 lililopo eneo la TIPER Kigamboni kwa ajili ya kuhifadhi mafuta.

"TPDC itakamilisha taratibu za upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa matangi matatu ya kuhifadhi mafuta katika eneo la Kigamboni - Dar es Salaam. Serikali kupitia TPDC imetenga Sh. bilioni 17.1 kwa ajili ya kazi hizo," alisema.

Baadhi ya miradi itakayotekelezwa katika mwaka ujao wa fedha ni pamoja na wa gesi asilia Kinyerezi I Extension (MW 185) na kusaka fedha kwa ajili ya miradi ya maji Ruhudji (MW 358), Rumakali (MW 222), Kikonge (MW 321), Maragalasi (MW 49.5), Kakono (MW 87.8), Jua Shinyanga (MW 150), gesi asilia mawe (MW 150) na ukarabati wa Kituo cha Kufua Umeme cha Hale Hydro Power Plant uliotengewa Sh. bilioni 6.4.

Akiwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Nishati, Mwenyekiti wake, Luka Kitandula, aliipongeza wizara hiyo kwa mafanikio yaliyopatikana katika uongozi wa Rais Samia na Waziri January.

Alipendekeza kazi kubwa ifanyike kubaini makandarasi wasiotimiza makubaliano yao katika miradi ya Wakala wa Umeme Vijijini (REA).

***Imeandaliwa na Elizabeth Zaya na Romana Mallya***

# Dk. Mwinyi azindua Kamati ya Maridhiano kumaliza uhasama

**Na Mwandishi Maalum,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesisitiza dhamira yake ya kuiunganisha Zanzibar kuwa moja, yenye amani, upendo, maridhiano na mshikamano.

Ikulu, Zanzibar jana, Rais Dk. Mwinyi alisisitiza dhamira yake hiyo alipozindua Kamati ya Maridhiano kati ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na ACT-Wazalendo ili wafanye kazi pamoja kuendeleza amani iliyopo nchini.

Alisema bado ana nia ya kuiendeleza Zanzibar kuwa moja bila kujali rangi, asili, imani za dini, au itikadi za kisiasa kama alivyoahidi kwa mara ya kwanza alipohutubia Baraza la Wawakilishi Novemba mwaka jana kuhusu dhamira yake ya kuwaunganisha wananchi wa Zanzibar kuwa wamoja.

Alisema kuwa baada ya uchaguzi wa mwaka 2020 waliendeleza tena Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar kama ilivyoelekeza, kwa nia ya kuweka jukwaa la kutafuta suluhu ya kudumu ili kujenga maridhiano endelevu na amani ya kudumu Zanzibar.

Rais Dk. Mwinyi aliitaja ni njia pekee ya kujenga uchumi imara, kuondoa umaskini na kujenga nchi kwa ustawi wa wananchi.

Alitumia fursa hiyo kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia kwake kwa vitendo azma ya kuleta maridhiano ya kisiasa nchini ikiwamo kuunda kikosi kazi kilichopitia ripoti ya mkutano wa Baraza la Vyama vya Siasa na kutoa mapendekezo.

Pia alimshukuru Rais Samia kwa uzalendo wake wa kufanya vikao na viongozi wa vyama vya siasa kwa kusikiliza maoni yao na kuyafanyia kazi.

Dk. Mwinyi ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar, alikishukuru Chama cha ACT-Wazalendo kwa kukubali kukaa pamoja na viongozi wa CCM ili kuendeleza dhamira ya kushirikiana na kuimarisha umoja wa kitaifa.

Mwaka 2010 kuliwahi kuundwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kufuatia mifarakano ya kisiasa na jamii ikiwamo kuzorota kwa amani baada ya kuundwa kwa vyama vingi vya siasa mwaka 1992 ambapo tangu uchaguzi mkuu wa mwaka 1995 na miaka iliyofuata, Zanzibar ilikumbwa na fujo za kisiasa na amani kudorora.

Kufuatia marekebisho ya 10 ya Katiba ya Zanzibar, mwaka 2010 kuliundwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ili kuendeleza amani ya kudumu.

Hafla ya uzinduzi wa Kamati ya Maridhiano baina ya CCM na ACT- Wazalendo ilihudhuriwa na viongozi wakuu na wajumbe kutoka vyama viwili hivyo wakiwamo Makamu Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo Zanzibar ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM ambaye ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Muhamed Said Dimwa na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM, Dk. Khalid Salum Muhamed ambaye ni Waziri wa Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi.

Wengine kutoka CCM; Vuai Ali Vuai, Naibu Katibu Mkuu CCM, Najma Murtaza Giga na Salum Hassan Bakari. Kutoka ACT-Wazalendo ni; Naibu Katibu Mkuu ambaye ni Waziri wa Afya wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, Omar Said Shaaban, Mwanasheria Mkuu wa ACT ambaye ni Waziri wa Biashara, Mansour Yussuf Himid na Ismail Jussa Ladhu ambaye ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya ACT-Wazalendo.



Fundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA), Hamad Seif, akiboresha huduma ya maji katika bomba la inchi sita eneo la Tabata Shule jijini Dar es Salaam jana. Kukamilika kwa kazi hiyo kutanufaisha wateja zaidi ya 1,700 wa maeneo ya Tabata Shule, Umoja Road, Tabata Bima, Muslim na Magengeni. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Waangua kilio kwa Chongolo kisa mradi

**Na Nebart Msokwa,** IRINGA

WANANCHI wa Kata ya Uhambingeto, Wilaya ya Kilolo mkoani Iringa, wameangua kilio mbele ya Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo (pichani), wakilalamikia kutokamilika mradi wa maji zaidi ya miaka 10 licha ya mkandarasi kulipwa huku akiwa hajulikani alipo.

Wananchi hao waliangua kilio hicho jana wakati Chongolo alipofanya ziara kwenye kata hiyo ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya siku sita mkoani hapa yenye lengo la kukagua utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya chama hicho, kuwasikiliza wananchi na kuangalia uhai wa chama.

Diwani wa kata hiyo, Tulimtwa Mlanga, alimlalamikia mkandarasi anayetekeleza mradi huo ambaye ni Mshamindi Construction, kutokamilisha mradi huo huku wananchi wakihangaika kupata huduma hiyo.

Alisema wananchi wa eneo hilo wamekuwa wakitegemea maji ya kwenye mabwawa ambayo kipindi cha kiangazi yanakauka na kuwafanya wawe wanasafiri umbali mrefu kufuata huduma hiyo.

Hata hivyo, alisema maji ya mabwawa ambayo huyatumia usalama wake ni mdogo kiafya na kwamba waliamini mradi huo ndiyo ungekuwa mkombozi kwao.

Alisema mradi huo umefikia asilimia 55, lakini alishalipwa asilimia zaidi ya 50 na wamekuwa wakimfuatilia bila mafanikio kutokana na mkandarasi huyo kutojulikana alipo.

"Mimi pamoja na baadhi ya wajumbe tulikwenda mpaka Dodoma bahati mbaya hatukuonana na Waziri wa Maji ambaye ndiye tulitaka kuonana naye, mbunge wetu alitusaidia kumpigia simu ila bado tatizo ni kubwa," alilalamika Tulimtwa.

Pia, alisema mradi huo utakapokamilika utaondoa kero ya wananchi kulipa gharama kubwa kununua maji kwa sasa wananunua Sh. 1,000 kwa ndoo ya lita 20.

Mbunge wa Jimbo la Kilolo, Justine Nyamoga, alimuomba Katibu Mkuu Chongolo kuwasaidia kumchukulia hatua kali mkandarasi huyo.

Alisema kitendo cha wananchi kutumia maji machafu wakati mkandarasi alishalipwa fedha ni kutowatendea haki wao pamoja na serikali ambayo ndiyo iliyotoa fedha.

Nyamoga alisema, mkandarasi amekuwa mwiba kwa wananchi wa kata hiyo na kusababisha chuki kwa chama na serikali kutokana na ucheleweshwaji wa mradi huo.



"Ndugu katibu mkuu kuna miradi ya maji ambayo ilianza wakati huu unatekelezwa na imeshakamilika maji yanatoka, lakini ndiyo kama unavyoona, tunahitaji nguvu ya ziada ili kuokoa afya za wananchi," alisisitiza Nyamoga.

Katibu Mkuu Chongolo, alimuagiza Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, kwenda katika kata hiyo ndani ya wiki moja kuwasikiliza wananchi hao na kuchukua hatua dhidi ya mkandarasi anayetekeleza mradi huo.

Aidha, aliagiza Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira (RUWASA) Mkoa wa Iringa, kuchukua hatua za kisheria dhidi ya mkandarasi huyo.

Aliagiza mradi huo kuanza kutekelezwa na mamlaka hiyo kwa kutumia akaunti ya dharura na kwamba unatakiwa kukamilika ndani ya miezi mitatu.

"Mimi nataka Waziri wa Maji mwenyewe ndiye aje hapa awape pole, lakini pia aje afuatilia kinachomkwamisha mkandarasi huyu kukamilisha mradi na ikibainika kwamba kuna mtu anasababisha tutamchukulia hatua kali," alisema Chongolo.

Alisema serikali imekuwa ikitoa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, lakini baadhi ya watu wanakwamisha.

# ACT yazinyooshea kidole shida kuu 5

**Na Julieth Mkireri,** MPANDA

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimetaja mambo matano yanayowasumbua Watanzania, ukiwamo ugumu wa maisha kutokana na kupanda kwa bei za bidhaa na kilimo kutokupewa nafasi kubwa katika mipango ya nchi licha ya kuajiri asilimia 67 ya wananchi.

Mengine yanayonyooshewa kidole na chama hicho ni uhaba wa ajira kwa wenye sifa ya kuajiriwa, vikwazo katika kupata huduma bora za afya, elimu kutokufanywa kama nyenzo ya ukombozi pamoja na kukithiri kwa umaskini uliopitiliza.

Mwenyekiti wa Chama hicho, Juma Duni Haji, alibainisha hoja hizo alipozungumza na wananchi wa Mpanda mkoani Katavi katika mwendelezo wa ziara ya viongozi wa chama hicho.

Duni alisema ACT-Wazalendo imefanya utafiti na kujiridhisha kuhusiana na masuala hayo matano kuwa ni mambo yanayowasumbua Watanzania na serikali imekosa mbinu sahihi za kuwanasua.

Alisema ni wakati mwafaka sasa na kwa Watanzania kuachana na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kuwa katika miaka zaidi ya 60 ya uhuru kimeshindwa kutatua vikwazo hivyo.

"Sisi ACT tukishasema mkitupa ridhaa tutakwenda kufanya mapinduzi katika kilimo ambacho kinaajiri asilimia 67 ya Watanzania na tunafahamu tukileta mapinduzi katika kilimo, tutakuwa tumepiga hatua kubwa juu ya kuyaondoa masuala hayo yanayowasumbua Watanzania," alisema.

Duni pia alisema chama hicho kinaitaka serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ili ununue mazao.

Mwenyekiti huyo alisema chama hicho kilifanya utafiti na kubaini robo tatu ya Watanzania hasa wa mjini kilio kikubwa ni gharama za maisha kuwa kubwa zikichangiwa na bei za vyakula.

"Tunataka NFRA iwe na uwezo wa kuweka chakula mpaka tani milioni tatu za mahindi, mpunga, uwele mtama na maharage ili kuwe na chakula cha akiba ambacho ikitokea lolote Watanzania hawawezi kukumbwa na njaa angalau kwa miezi mitatu," alisema.

Kiongozi wa chama hicho, Zitto Kabwe, alieleza kukithiri kwa migogoro ya ardhi katika Mkoa wa Katavi kati ya halmashauri na wananchi, pia wananchi na mamlaka za hifadhi.

Alieleza chanzo cha migogoro ni kasi ndogo ya upangaji wa miji na kukosekana kwa eneo la kutosha kwa ajili ya malisho ya mifugo. Alitaja sababu zaidi za migogoro hiyo ni ardhi kuwa chanzo cha mapato ya halmashauri.




# PM ataka jitihada akiba ya mafuta miezi mitano

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI Mkuu, Kasimu Majaliwa ameitaka kampuni ya kuhifadhi mafuta Tanzania (TIPPER), kuweka mipango ambayo itawezesha nchi kuwa na akiba ya mafuta ya miezi mitano hadi sita.

Majaliwa alitoa kauli hiyo jana wakati akizindua wiki ya maonyesho ya Nishati yanayofanyika katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma.

Aliiataka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), kuratibu suala hilo ili lifanikiwe.

"Tumepata taarifa hali ya utafutaji mafuta, inaendelea vizuri na waendeshaji wa mitambo msiwe na wasiwasi. Tunataka kuhakikisha kwamba tunajenga uwezo wa kuwa na mafuta ya miezi mitano mpaka sita. Tunatakiwa kujenga maeneo mapya kwa kuweka mipango ya nchi hii itakayokuwa na uwezo wa kuhifadhi mafuta," alisema Majaliwa.

"TIPPER waweke mipango ya kuhifadhi mafuta, tafuteni matangi mengine zaidi ya yale yaliyopo, EWURA hili ni lenu nataka mliratibu."

Kuhusu dira ya taifa ya matumizi ya nishati safi, Majaliwa alisema mwelekeo wa serikali kwa sasa ni matumizi ya nishati hiyo na hakuna kurudi nyuma na kwamba tayari wameunda kamati ya kitaifa inayoratibu utoaji wa elimu kwa ajili ya matumizi yake pamoja na namna wajasiliamali wanavyotakiwa kuchangamkia fursa hiyo.

"Tumeunda kamati ya kitaifa inayoratibu utoaji elimu na kuonyesha fursa za wajasiriamali watakaohitaji kuingia katika sekta hii, tunawataka Watanzania kubadilika kwa kutumia nishati mbadala ili kuepukana na athari za mabadililo ya tabianchi," alisema Majaliwa.

Alisema matumizi hayo ya nishati safi yataanza na taasisi zinazokaliwa na watu zaidi ya 100 ikiwamo za elimu, vyuo vya jeshi, makambi na mengineyo.

"Tunataka hizi zote zianze kutumia nishati hiyo na ndiyo mwelekeo wa taifa letu, tunataka Watanzania tupike na tutumie majiko yanayotumia nishati mbadala."

Kuhusu mradi wa kutafuta gesi wa LPG wa mkoani Lindi, Majaliwa alisema umefikia hatua nzuri.

"Tumeoma miradi kadhaa ikiwamo wa kutafuta gesi, mradi huu umefikia hatua nzuri, nataka wananchi wakae tayari kuupokea," alisema Majaliwa.

"Niwapongeze watumishi katika wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya. Nafahamu kuna changamoto nyingi mnazokumbana nazo, ikiwamo maneno yanayozungumzwa, nyie chapeni kazi achaneni na maneno, huwezi kufikia mafanikio bila kupitia changamoto."

Waziri Nishati, January Makamba, aliwaomba wabunge kuhamasisha na kutoa elimu ya matumizi ya nishati safi ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira.




Kaimu Mkurugenzi wa Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Dk. Erasto Mlyuka (katikati), akiwa na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) Tanzania, Christine Musisi (kulia), Mkuu wa Umoja wa Ulaya (EU) Tanzania, Cedric Merel (wa pili kulia) na wadau wengine, wakizindua awamu ya pili ya ufadhili kwa wajasiriamali jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MAULID MMBAGA**

## Wengi hawana uelewa sheria, haki za kidigitali

**Na Mary Geofrey**

WATANZANIA wengi hawana uelewa kuhusu sheria na haki ya kidigitali, hali inayosababisha kuvunja sheria na kushindwa kuchukua hatua wanapofanyiwa vitendo visivyofaa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya The Launch Pad, Carol Ndosi, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari katika warsha ya Shirikisho la Wadau Wanaotetea Haki za Kidigitali nchini (Digital Rights Coalition).

Alisema katika utafiti wao umebaini kuna makosa mengi yanafanyika mtandaoni kutokana na watumiaji kutofahamu haki na wajibu kama raia wa kidigitali ikiwamo sheria zinazowalinda watumiaji, zinazolinda taarifa na makosa mengine anayofanyiwa mtandaoni.

Alitaja hatua za kuondoka na tatizo hilo ni kampuni za simu za mkononi kutoa elimu kupitia simu zao pindi mteja anaponunua akutane na elimu ya kudhibiti uhalifu wa mitandaoni.

Alisema zipo jitihada zinazofanywa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Jamii Forums na Launch Pad ambao wamekuwa wakielimisha jamii kuondokana na utapeli, pia matumizi salama ya mitandao.

Alisema kupitia Wizara ya Habari, Teknolojia ya Habari na Mawasilino, serikali imetenga fungu kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma.

Kuhusu picha za utupu kusambazwa mitandaoni, alisema sheria haimlindi mwathirika wa makosa hayo na hivyo kumfanya mtoto wa kike kukosa ujasiri wa kuripoti kwa sababu mtuhumiwa wa kwanza ni yeye.

Meneja Programu wa JamiiForums, Ziada Seukindo, alisema shirikisho lilianza mwaka jana kwa ajili ya kufanya uchechemuzi wa haki za kidigitali, kuangalia sheria zinazowapa haki, pia kuangalia ukubwa wa jukwaa hilo unaoweka utu wa watu kuwa mitandaoni.

# Jalada kesi aliyemchoma mkewe larudishwa Kisutu

**Na Grace Gurisha**

JALADA la kesi ya mauaji inayomkabili mfanyabiashara Khamis Luwonga (38), anayetuhumiwa kumuua mkewe, Naomi Marijani na kumchoma moto kwa kutumia magunia mawili ya mkaa, limerudishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, kwa ajili ya usikilizwaji wa uamuzi kutoka Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam.

Mshtakiwa kupitia mawakili wake, Mohamed Majaliwa, Fatuma Abdul na Zidadi Mikidadi, aliwasilisha mahakamani hapo maombi ya kutaka kupata maelezo ya uhalali wa kesi ya mauaji namba 5, 2022, iliyopo Mahakama ya Kisutu na kumuachia huru mshtakiwa.

Katika uamuzi wa maombi hayo, Jaji Obadia Bwegoge, ambaye ndiye aliyeshikiliza maombi hayo, alisema kulingana na sheria inavyotaka, mahakama hiyo haina mamlaka ya kufanya uamuzi wa kumuachia huru mshtakiwa.

Aidha, alielekeza jalada la kesi hiyo lirudishwe Mahakama ya Kisutu ili hakimu anayeisikiliza shauri hilo atolee uamuzi kuhusu uhalali wa kuwapo kwa kesi hiyo ya mauaji katika mahakama hiyo.

Jalada hilo limesharudishwa mahakamani hapo na kupangiwa Juni 8, 2023, mshtakiwa atafikishwa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Ramadhani Rugemalila kwa ajili kusikilizwa kwa uamuzi wa Mahakama Kuu.

Jaji Bwegoge alisema, ametoa uamuzi huo kwa kuangalia majibu ya maswali mawili, kama maombi yaliyoletwa ni kweli sheria imevunjwa na la pili ni kama Mahakama Kuu ina mamlaka ya kutoa uamuzi wa maombi hayo.

Alisema kwa kujibu swali la kwanza la uhalali wa maombi hayo kisheria, sheria ipo wazi imeelekeza ni namna gani upande wa mashtaka unaweza kuamua kama hautakuwa na nia ya kuendelea na shauri.

"Sheria imesema kwamba upande wa mashtaka unaweza kuiandikia mahakama au kuiambia kwa mdomo kama haina nia ya kuendelea na shauri na mshtakiwa anatakiwa aachiwe huru kama yupo gerezani," alisema.

Pia, alisema kama upande wa mashtaka utamkamata tena mshtakiwa kwa kosa lile lile baada ya kuachiliwa, inatakiwa ushahidi ukamilike na siku ya kwanza anapoletwa mahakamani kesi isikilizwe.

"Lakini katika maombi haya mshtakiwa alikamatwa kwa kosa lile lile na ameshapandishwa mahakamani zaidi ya mara tano kwa kesi ya kutajwa," alisema.

"Hii inajidhihirisha katika rekodi zilizopo katika jalada la kesi ya inayoendelea Mahakama ya Kisutu. Hivyo basi upande wa mashtaka ni dhahiri umekeuka sheria," alisema Jaji Bwegoge.

Alisema katika swali la pili, kulingana na sheria, Mahakama Kuu haina mamlaka ya kufanya uamuzi wa kumuachilia mleta maombi, mshtakiwa aliomba hivyo kwa madai kuwa upande wa mashtaka hauna ushahidi wa kutosha wa kumshtaki.

"Kulingana na sheria ilitaka maombi haya yaombwe mbele ya mahakama iliyokuwa inaendesha kesi hiyo, naelekeza jalada lirudishwe Mahakama ya Kisutu na mheshimiwa anayesimamia kesi ya mleta maombi alitolee uamuzi juu ya uhalali wake," alisema.

Katika kesi hiyo ya muaji namba nne ya mwaka 2019, mshtakiwa Luwonga, mkazi wa Kigamboni, Dar es Salaam anadaiwa Mei 15, 2019 akiwa Gezaulole eneo la Kigamboni alimuua Naomi Marijani.

## TANGAZO


A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
KILIMANJARO
DRINKING WATER
FURAHIA MAISHA
NA MAJI ASILIA
500ml
1000ml
1500ml
6L
12L
18.9L
+255 659 536 937, +255 758 979 641, +255 659 785 276
kdw@bbl.co.tz
kilimanjarodrinkingwater
kilimanjaro_drinking_water

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uamuzi wa serikali kusitisha mikopo ya wanawake usichukuliwe mtazamo hasi

**HIVI** karibuni Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, imetangaza kusitisha utoaji mikopo ya Maendeleo ya Wanawake (WDF), ili kufanya maboresho na kuandaa utaratibu utakaowezesha fedha hizo kutolewa na benki.

Taarifa inayotolewa na kitengo cha mawasiliano serikalini cha wizara hiyo inaeleza mikopo hiyo ilikuwa ikitolewa na wizara kwa kushirikiana na mamlaka za serikali za mitaa bila gharama zozote za maombi kwa waliokidhi vigezo ili kuwawezesha wanawake kiuchumi na kupunguza unyanyasaji wa kijinsia majumbani.

Mikopo hiyo kama inavyoelezwa imekuwa na manufaa makubwa kwa wanawake walioitumia kwa malengo yenye tija kwa kuwaongeza kibiashara kuanzia mitaji na kukuza biashara zao hali iliyowainua na kuwatoa katika umaskini na kuwapandisha juu kiuchumi. Mafanikio hayo yaliipa serikali nguvu na matumaini ya kuendelea kutoa mikopo hiyo kupitia shuhuda za mafanikio yao, ikiwamo kusomesha watoto na kujenga makazi bora kupitia faida za biashara zao.

Lakini kuna kundi la pili la wanawake wasiojielewa, ambao wanaelezwa kuwa wameitumia vibaya fursa hiyo serikali kwa kuchukua mikopo hiyo na kufanya mambo ambayo si ya kuiwekezaji ambayo ni kinyume na makubaliano hali iliyochangia kuitia serikali hasara na hatimaye kufanya uamuzi huo.

Baadhi yao wamekuwa wakichukua mikopo hiyo na kuwaminisha maofisa mikopo ya halmashauri kuwa wanakwenda kuboresha biashara zao kinyume chake kuweka mikesha ya vigodoro, wengine kukesha kwenye kumbi za starehe ili mradi waonekane kuwa wana pesa mbele za wenzao matokeo yake wanashindwa marejesho na kuitia serikali hasara.

Yapo maelezo kuwa wapo wanawake wiki nzima wanavaa vijora vipya na kupita kuwatambia wenzao kuwa wamenunua nguo hizo kupitia mikopo ya serikali za mitaa, lakini ikifika wakati wa kulipa marejesho wanakimbia nyumba na kuwapa wanakikundi wenzao tabu ya kumtafuta au kumlipia rejesho.

Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2021/2022, inaonyesha kuwa Sh. bilioni 88.42 zilizotolewa kama mikopo kwa makundi ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu katika mamlaka za serikali za mitaa 180 hazikurejeshwa.

Aidha, taarifa hiyo inaeleza kuwa kutorejeshwa kwa mikopo hiyo kumechangiwa na wahusika kutochukuliwa hatua kali za kisheria zitakazowasukuma walazimike kurejesha mikopo hiyo na kukosa elimu ya kufanya marejesho.

Tunapongeza uamuzi wa serikali kusitisha utaratibu wa mikopo hiyo na kuamua kazi hizo sasa zifanywe na benki kwa kuwa huko kutakuwa na utaratibu maalum wa kuwabana wanawake hao na kufuatilia urejeshaji na usimamizi utakaowezesha kila mmoja kujua kuwa fedha hizo si zawadi.

Kwa kawaida mikopo ya benki ina ukomo wa uvumilivu wa kutolipa deni, ikifika muda uliowekwa benki, maofisa watalazimika kupiga mnada thamani ulizoandikisha kama dhamana hata kwa bei ya hasara ili kufidia deni lao.

Tusingependa kinamama wafike huko ili kinachohitajika sasa ni kuwasaidia ambao wanatamani kuendeleza maisha yao, lakini wanakwamishwa na wachache wasiokuwa na nia ya dhati ya kujiletea maendeleo.

Tunapenda kushauri kuwa wakati umefika kwa serikali kuandaa miundombinu ikiwamo sehemu za kufanyia biashara, maeneo ya kilimo, viwanda vidogo na vya kati kwa kutumia fedha za maendeleo ya wanawake, vijana na wenye ulemavu na kuwaweka wanufaika hao kwenye maeneo hayo ili kuzalisha kwa faida itakayowanufaisha wao na pia kulipa gharama za miundombinu ambazo ni mikopo hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Sheria zifanye kazi yake kuokoa afya za ndugu wasiovuta tumbaku

**JANA** ilikuwa ni kilele cha maadhimisho ya Siku ya Kuzuia Tumbaku Duniani, ambayo mwaka huu yalibeba kaulimbiu "Tunahitaji chakula, sio tumbaku".

Ni kaulimbiu inayolenga kuongeza uelewa wa uzalishaji mazao mbadala na fursa za masoko kwa wakulima wa tumbaku, wakiwahimiza kulima mazao endelevu na yenye lishe.

Mei 31 ya kila mwaka ni kilele cha maadhimisho yanayoambatana na kaulimbiu tofauti, ikiwa ni kampeni ya kuiepusha jamii dhidi ya uvutaji sigara na aina nyingine ya tumbaku.

Hadi sasa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), nayo imekuwa na mikakati yenye lengo la kudhibiti matumizi ya sigara, ili kulinda afya za Watanzania.

Mojawapo ya mikakati hiyo, ni kutoa elimu katika jamii iache kutumia tumbaku na kusimamia sheria ya kuwa na sehemu ya kuvutia sigara, hata bidhaa nyingine za tumbaku.

Mamlaka hiyo inatoa elimu kwa jamii, kuwa uvutaji una madhara ya kansa ya damu, mapafu, huku ikiwataka wanaovuta ama kuacha au kupunguza matumizi ya tumbaku.

TMDA pia inachukua hatua hiyo, kutokana na kinachoelezwa kuwa sheria inazuia uvutaji kwenye mkusanyiko wa watu na inaelekeza, kutenga sehemu ya kuvuta, ili kutowavutisha wale wasiovuta.

Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Adam Fimbo, ameshatamka kuwa watakaoshindwa kuzingatia hayo na kuvuta katika mkusanyiko wa watu, sheria itachukua mkondo wake.

Katika ufafanuzi wake, anasema awali hakukuwapo chombo cha kudhibiti tumbaku na kwamba kazi yao ni kutoa elimu zaidi wakiachana na kukamatana, ili jamii iache matumizi ya tumbaku na bidhaa zake.

TMDA inatoa angalizo kwa watu wenye umri chini ya miaka 18 kutojiingiza katika matumizi ya tumbaku, ingawaje katika uhalisia, ukiukwaji wa kanuni hiyo uko juu zaidi.

Mtu anapozuru maeneo mbalimbali, kama kumbi za starehe maeneo mengine ya mkusanyiko wa watu kama vituo vya mabasi, masoko na kwingineko, hali ni ile,wasiovuta wanavutishwa bila kupenda.

Kwa mfano, mtu anavuta sigara kwenye mkusanyiko wa watu, moshi wake unasambaa hadi kwa wasiovuta, hivyo kuwavutisha bila wao kupenda, kitendo ambacho kinaweza kuchangia kuathiri afya zao.

Wataalamu wa afya wanaeleza kuwa mvutaji sigara akivuta na akipuliza moshi, madhara yake huwakuta wote na yule aliyevuta hewa moshi huo na hivyo kumweka katika mazingira ya hatari kiafya.

Ili kulinda afya za wasiovuta, ndio maana kuna maelekezo ya kutenga sehemu za kuvutia sigara, ingawa ingekuwa ni vyema hata wavutaji wakaangalia uwezekano wa kulinda afya zao.

Inaelezwa kuwa, matumizi ya tumbaku huathiri afya ya mtu kwa njia nyingi na kusababisha magonjwa mengi, ikiwamo kuongezeka hatari ya maambukizi ya ufizi na kupoteza meno.

Vilevile inaelezwa, matumizi ya tumbaku yanasababisha kupungua kwa hisia ya harufu na ladha, kuzeeka mapema kwa ngozi, kuongezeka hatari ya kuzorota kwa seli zinazohusiana na umri.

Katika mazingira hayo, inaelezwa inatoa nafasi kusababishia mvutaji upofu, hivyo ni vyema kila mtu akawa makini kulinda afya yake, kwa kuzingatia elimu inayotolewa na TMDA.

Elimu hiyo inapozingatiwa, inatajwa kuweza kuwaokoa watu wengi wakiwamo watoto wadogo ambao wamekuwa wakivutishwa na wazazi wao wakiwa katika vyombo binafsi vya usafiri au hata wakiwa wamebebwa.

Wanajamii tunaweza kuhojiana, ni kwanini hilo? Sababu ni wazi, wapo baadhi ya wazazi huvuta sigara katika magari yao wakiwa na watoto, wengine wanawapakata watoto, huku wakivuta sigara, kitendo ambacho ni rahisi watoto kuvutishwa moshi.

# CRDB yatwaa tuzo ya Benki Bora A. Mashariki

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imewashukuru wateja na wadau wake kwa kutunukiwa tuzo ya Benki Bora Afrika Mashariki na jarida maarufu la masuala ya benki, fedha na uchumi la African Banker katika hafla iliyofanyika jijini Sharm El Sheikh, Misri.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alitoa shukrani hizo wakati akiipokea tuzo hiyo kutoka kwa na Meneja Mwandamizi wa Ubia na Ushirikiano wa Kimkakati, Masele Msita, aliyekuwa sehemu ya wafanyakazi walioiwakilisha benki hiyo katika hafla ya tuzo iliyofanyika Mei 24 mwaka huu.

Akizungumza kuhusiana na tuzo hiyo ofisini kwake Makao Makuu ya Benki jijini Dar es Salaam, Nsekela alisema wateja wa benki hiyo wamekuwa sehemu ya mafanikio ya utekelezaji wa mikakati mbalimbali ya biashara ambayo imeleta mageuzi ya biashara na kupelekea kupata tuzo hiyo.

"Niwashukuru wateja wetu, wanahisa, serikali, Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na washirika wetu wa biashara kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakitupatia na kuendelea kutufanya kuwa bora zaidi. Hii sio tuzo ya Benki ya CRDB peke yake, ni tuzo ya watanzania wote," alisema Nsekela.

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Benki ya CRDB imefanya mageuzi makubwa katika biashara yake, ambayo yamesaidia katika kutengeneza thamani endelevu, kuongeza ujumuishi wa kifedha na kujenga uchumi jumuishi kupitia bidhaa, huduma na mifumo bunifu ya kidijitali ya utoaji huduma ikiwamo SimBanking.

"Tuzo hii inathibitisha mafanikio ya mkakati wetu wa biashara uliopita wa 2018 – 2022, na nafasi ya Benki ya CRDB kama 'Benki Kiongozi' nchini. Vilevile, inaonyesha mwanga katika utekelezaji wa mkakati wetu mpya wa biashara wa 2023–2027 ambao unasisitiza katika mageuzi thabiti yanaoyolenga kuboresha maisha ya watu wetu na uchumi wetu," alisema.

Benki ya CRDB inatazamiwa kuwa na mchango mkubwa zaidi katika kuchochea ukuaji wa uchumi wa ukanda huu wa Afrika Mashariki baada ya kupata kibali cha kuanzisha kampuni tanzu katika nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC). Benki hiyo pia hivi karibuni ilikuwa benki ya kwanza nchini kuanzisha kampuni kamili ya bima, CRDB Insurance Company Ltd.

Katika kinyang'anyiro cha tuzo hiyo, Benki ya CRDB imewabwaga wapinzani sita iliyokuwa ikishindana nao ambao ni Afreximbank, Bank of Africa, Co-operative Bank ya Kenya, Mauritius Commercial Bank, Trade and Development Bank na Trust Merchant Bank ya DRC.

Hafla ya ya utoaji tuzo hizo ilikwenda sambamba na mkutano mkuu wa mwaka wa Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Benki ya CRDB ikiwakilishwa na Meneja Mwandamizi wa Ubia na Ushirikiano wa Kimkakati, Masele Msita, ikishiriki mdahalo wa African Banker uliozungumzia jitihada za benki barani Afrika kuziwezesha biashara zinazomilikiwa na kuongozwa na wanawake wajasiriamali na programu ya AFAWA.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, akipokea tuzo ya 'Benki Bora Afrika Mashariki' kutoka kwa Meneja Mwandamizi wa Ubia na Ushirikiano wa Kimkakati wa Benki ya CRDB, Masele Msita, jijini Dar es Salaam jana iliyotolewa na Jarida la African Banker katika hafla za tuzo zilizofanyika wakati wa Mkutano Mkuu wa Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Sharm El Sheikh, nchini Misri mwishoni mwa wiki iliyopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hukumu kesi kupinga ma-DED kusimamia uchaguzi mkuu yaiva

**Na Enock Charles**

KESI ya kupinga wakurugenzi wa halmashauri kusimamia uchaguzi nchini kwa niaba ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) inatarajiwa kutolewa uamuzi Juni 13 mwaka huu katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu (ACHPR).

Shauri hilo lilifunguliwa na Mkurugenzi wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Bob Wangwe.

Awali Mahakama ya rufani nchini ilitengua uamuzi wa Mahakama Kuu iliyozuia wakurugenzi kusimamia uchaguzi katika uamuzi wa Mahakama Kuu uliotolewa mwaka 2019.

Mahakama hiyo ilifuta sheria iliyokuwa inawapa wakurugenzi wa halmashauri mamlaka ya kuwa wasimamizi wa uchaguzi uamuzi ambao ulilazimisha NEC kuteua watu wake badala ya kutegemea wateule wa Rais, jambo ambalo linapingwa vikali na baadhi ya wadau wa katiba.

**Pia ilibatilisha kifungu 7(3) kinachoipa NEC mamlaka ya kuteua mtu yeyote miongoni mwa watumishi wa umma kuwa msimamizi wa uchaguzi.**

Uamuzi uliotolewa na Mahakama ya Rufani Oktoba 2019 uliruhusu wakurugenzi kusimamia uchaguzi na kutengua uamuzi wa Mahakama Kuu uliozuia.

Jopo la Majaji wa Mahakama ya Rufani likiongozwa na Jaji Augustine Mwarija lilikubaliana na hoja ya wakata rufani (serikali) kuwa kusema wakurugenzi ni wateule wa Rais, hivyo kushindwa kufuata taratibu ni ya kufikirika.

Majaji wengine katika jopo hilo walikuwa ni Stella Mugasha, Richard Mziray, Rehema Mkuye na Jacob Mwambegele.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi Bob Wangwe alisema hawakuridhika na uamuzi wa Mahakama ya Rufani kubatilisha uamuzi wa Mahakama Kuu ambayo ilizuia wakurugenzi kusimamia uchaguzi, hivyo waliamua kwenda mbele zaidi katika mahakama hiyo ya Afrika. Sasa wamepewa taarifa uamuzi utatolewa Juni 13 mwaka huu.

"Tumepokea taarifa kuhusu ile kesi yetu ya kupinga wakurugenzi kusimamia uchaguzi ambayo tuliifungua Mahakama ya Afrika mwaka 2020 ili kuboresha mifumo yetu ya uchaguzi. Itatolewa uamuzi Juni 13 mwaka huu, ni imani yetu tutapata uamuzi sahihi," alisema Wangwe.

Mei 11 mwaka 2019, Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam ilibatilisha kifungu 7 (1) cha Sheria ya Uchaguzi kinachoiruhusu NEC kuwateua wakurugenzi wa majiji, manispaa za miji kuwa wasimamizi wa uchaguzi.

Pia ilibatilisha kifungu 7(3) kinachoipa NEC mamlaka ya kuteua mtu yeyote miongoni mwa watumishi wa umma kuwa msimamizi wa uchaguzi.

Hukumu hiyo ilitolewa na jopo la majaji watatu; Dk. Atuganile Ngwala, Dk. Benhajj Masoud na Firmin Matogolo.

## KABWELA

Na Fadhil Mohammed



# DC Jokate azindua kampeni kusimamia miradi maendeleo

**Na Beatrice Shayo**

MKUU wa Wilaya ya Korogwe mkoani Tanga, Jokate Mwegelo, amezindua kampeni itakayosimamia miradi ya maendeleo kukamilika kwa wakati na kuondoa hujuma zitakazofanywa na watumishi.

Kampeni hiyo ilizinduliwa jana wakati wa ujenzi wa nyumba ya walimu katika Shule ya Msingi Magila Gereza iliyopo wilayani huko na pia kuwawezesha wananchi kuifahamu miradi inayotekelezwa na serikali.

"Tumezindua kampeni ambayo tumeita Operesheni Samia Maliza Miradi Wilaya ya Korogwe, ikiwa ni sehemu za jitihada za uongozi wa wilaya kutoa hamasa kwa watumishi na wasimamizi wa miradi kwa ngazi mbalimbali kuanzia halmashauri, kata, tarafa vijiji hadi vitongoji," alisema.

Alisema lengo ni kuisemea miradi hiyo kwa wananchi kwa kuwashirikisha na kuhakikisha inatekelezwa kwa miongozo ambayo inatolewa na serikali.

Mwegelo alisema lengo ni miradi itekelezwe kwa wakati, kwa kuzingatia thamani ya fedha iliyoingizwa kwenye miradi ikaonekane.

"Pia wananchi waweze kujua nini kinafanywa na serikali yao kwa ajili yao hatupendi kuona serikali inatumia fedha nyingi kwenye kuboresha miundombinu kwa sekta muhimu zinazogusa maisha ya wananchi kwa kawaida kama elimu, afya, barabara, maji na umeme zinachezewa ama kuhujumiwa na baadhi ya watumishi."

Mwegelo alisema lengo lao kubwa ni kutengeneza timu moja ya viongozi kutoka serikalini na chama kusimamia miradi hiyo na kuhakikisha inamalizwa kwa wakati.

# Vipuri vyakwamisha majaribio SGR

**Na Jenifer Gilla**

SERIKALI imetaja kiini cha kuchelewa kwa majaribio ya treni ya kisasa (SGR) kati ya Dar es Salaam na Morogoro yaliyokuwa yafanyike Mei, mwaka huu, kuwa ni kuchelewa kwa vipuri kutoka Canada kwa sababu ya UVIKO-19.

Awali serikali ilisema kuwa hayajafanyika kutokana na vichwa vya treni hizo kuchelewa kufika nchini mwezi Aprili, mwaka huu, kama ilivyotarajiwa.

Mkurugenzi wa Idara ya Habari-Maelezo na Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa vichwa hivyo havikufika nchini kwa wakati kutokana na mkandarasi aliyepewa kazi hiyo kukosa baadhi ya vipuri vinavyotumika kutengenezea.

Msigwa alitaja sababu za kukosekana vipuri hivyo ni viwanda vinavyotengeneza kutoka Canada kuyumba kutokana na janga la UVIKO-19 na vita vya Russia na Ukraine, vilivyosumbua dunia na kusababisha mtikisiko kiuchumi.

Aidha, Msigwa alisema mkandarasi huyo ameahidi kuwa kichwa cha kwanza cha treni hiyo kitakamilika Julai, mwaka huu na kitakapoingia nchini wataanza majaribio wakati wanaendelea kusubiri kichwa cha pili.

"Kwa hiyo nipo hapa kuwaambia Watanzania kwamba ni kweli tumeshindwa kuanza majaribio kama ambavyo tulipanga kwa sababu vichwa havijafika kwa wakati na serikali inaendelea kufuatilia kwa karibu ukamilishwaji wa vichwa hivi ili vitakapofika mara moja tuanze majaribio ya treni ya abiria," alisema Msigwa.

Alisema mabehewa sita kati ya 30 kutoka kwa mkandarasi huyo ambayo ni ya ghorofa, yameshakamilika na yanategemewa kuingia nchini Juni 2 au 3, mwaka huu na 24 yaliyobaki yataendelea kuja kwa awamu mpaka yatakapokamilika.

Alisema Februari 25, mwaka jana, Shirika la Reli Tanzania (TRC), lilivunja mkataba na kampuni ya Eurowagon ya nchini Uturuki baada ya kushindwa kutengeneza vichwa hivyo na mabehewa yake 30 kama walivyokubaliana na kuipa tenda hiyo mkandarasi wa sasa kutoka Ujerumani.

Aidha, alisema mabehewa 14 kati ya 59 waliyonunuliwa kutoka Korea yameshafikishwa nchini na mengine 45 yapo njiani wakisubiri vichwa vyake, huku mabehewa yaliyoagizwa kutoka China yanatarajiwa kuingia nchini mwakani.

Machi 21, mwaka huu, Mkurugenzi Mtendaji wa TRC, Masanja Kadogosa, aliwaambia Wajumbe wa Baraza Kuu la Wanawake wa CCM kuwa treni hiyo ilitarajiwa kuanza majaribio ya safari kwa kipande kilichokamilika bila abiria mwishoni mwa mwezi Aprili au mwanzoni mwa mwezi Mei, mwaka huu.



Ofisa Wanyamapori Msaidizi wa Wilaya ya Rufiji, Theresia Moshi, akielezea jinsi mamba anayedaiwa kuua mwanaume anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka 42 alivyouawa wilayani humo, mkoani Pwani juzi. Chini ni ngozi ya mamba huyo baada ya kuchunwa. **PICHA: BEATRICE MOSES**

# BoT yatoa maelekezo mapya biashara ya Dola

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imetoa maelekezo mapya kuhusu miamala yote ya fedha za kigeni inayozidi thamani ya dola za Marekani milioni moja kwa muamala mmoja katika soko la rejareja, lazima ifanyike kwa bei ya soko la fedha za kigeni baina ya benki.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa umma jana, BoT imesema miamala yote ya mteja mmoja kwa siku itajumlishwa, ili kujua jumla ya kiasi husika, lengo likiwa kulinda utulivu wa uchumi mpana na uthabiti wa mfumo wa kifedha nchini.

Katika sekula yake kwa taasisi hizo zinazojihusisha na biashara ya fedha za kigeni, Gavana wa BoT, Emmanuel Tutuba, alisema ni marufuku kufanya biashara ya fedha za kigeni na madalali wa kimataifa wa fedha za kigeni ambao hawajasajiliwa ndani ya Tanzania.

"Madalali/wafanyabiashara wa fedha za kigeni nchini wanatakiwa wakati wote kuzingatia utaratibu wa kumtambua mteja (KYC) kabla ya kufanya naye biashara hiyo," alisema.

Katika maelekezo hayo, kiwango cha juu cha mizania kati ya mali na amana katika fedha za kigeni (foreign exchange Net Open Position (NOP)) kitakuwa asilimia 10 ya mtaji wa msingi (core capital) na kinatakiwa kuzingatiwa wakati wote.

Alielekeza pia kwamba Barua za Udhamini (Letters of Credit (LCs)) za shehena zinazopitia nchini (transit cargoes) zitatokana na fedha za kigeni kutoka katika nchi ambako shehena hizo zinakwenda.

"Inasisitizwa kwamba uzingatiaji wa matakwa yaliyoainishwa hapa ni wa lazima na kutakuwa na usimamizi na ukaguzi kutoka BoT. Kukiuka maelekezo haya kutasababisha adhabu kama zinavyoelezwa katika Sheria ya Fedha za Kigeni ya Mwaka 1992," alieleza Gavana Tutuba.

Pia utekelezaji wa maelekezo ya uendeshaji wa huduma za fedha za kigeni kulingana na mahitaji ya sasa ya soko unaanza rasmi Juni Mosi mwaka huu.

Tutuba alisema maelekezo mapya ya Mei 31, mwaka huu yanafuta maagizo yaliyotolewa na BoT Agosti 6, mwaka 2020.

"Benki inawakumbusha wahusika wote wa huduma za fedha za kigeni kuzingatia matakwa ya mpango wa fedha za kigeni nchini muda wote," alielekeza Gavana.



# TSB yaanza kuwanoa wanafunzi kulima mkonge

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

BODI ya Mkonge nchini (TSB), imeanza kuelekeza nguvu zake kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, kupenda kulima zao hilo lenye tija kibiashara kwa kuwa mahitaji yake katika soko la nje ni makubwa kuliko uzalishaji.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mkonge na Masoko, Olivo Mtung'e, alisema uamuzi huo unalenga kuhamasisha uzalishaji wa zao hilo kwa ngazi ya familia kuanza ekari moja hadi tatu.

Alizungumza hayo jana baada ya kuzinduliwa kwa klabu ya kwanza ya kuhamasisha uzalishaji wa mkonge ya Shule ya Sekondari ya Coastal iliyoko jijini Tanga.

"Nchi nyingi sasa zinahitaji mkonge, lakini kiasi ambacho tunakilima ni kidogo, ndiyo maana baada ya kutengeneza wakulima wadogo; sasa tunahamasisha na sisi kwenye familia zetu, wenye mashamba ya ekari moja hadi tatu, walime mkonge ili kuimarisha uchumi wa familia," alisema.

Kutokana na hali hiyo, Mtung'e, alisema wahitimu wa shule za sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu, hawana haja ya kutafuta ajira kwa sababu mkonge wenyewe ni ajira, ukishapanda ndani ya miaka mitatu, unaanza kuvuna kwa muda wa miaka 18 mfululizo.

Wakati anazindua klabu hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa TSB, Saddy Kambona, alisema klabu hizo zitafundisha vijana hao kuhusu kilimo cha mkonge na sekta nzima ya mkonge kwa ujumla, kitu ambacho kitawawezesha kujiajiri baada ya kuhitimu masomo yao.

Alisema: "TSB tulilitazama wazo la kuwa na klabu za mkonge, kwa kuwa kuna kauli mbiu ya mkonge ni Tanga na Tanga ni mkonge; basi tunataka mtu akifika Tanga aone kweli kwamba mkonge ni Tanga. Tunategemea aone mkonge ndiyo zao kuu la kibiashara.

Aliongeza: "Sasa sehemu ya kuanzia ni kuwa na klabu za kuhamasisha, siyo tu kilimo cha mkonge, bali pia matumizi ya bidhaa za mkonge."

**Nchi nyingi sasa zinahitaji mkonge, lakini kiasi ambacho tunakilima ni kidogo, ndiyo maana baada ya kutengeneza wakulima wadogo; sasa tunahamasisha na sisi kwenye familia zetu, wenye mashamba ya ekari moja hadi tatu, walime mkonge ili kuimarisha uchumi wa familia.**

# Kairuki ang'aka madiwani kutumia whatsapp kudai posho

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angelah Kairuki, amechukizwa na kitendo cha madiwani kuhamasishana kudai nyongeza ya posho za kila mwezi kupitia mtandao wa kijamii wa whatsapp.

Alitoa kauli hiyo jana alipokutana na wajumbe wa Jumuiya ya Serikali za Mitaa Nchini (ALAT) jijini Arusha.

"Hivi kweli tunadai posho kupitia whatsapp na kuunda kamati itakayokwenda kwa Mheshimiwa Rais (Dk. Samia Suluhu Hassan) ili kudai kuongezewa posho?

**Nauliza haya kwa nia njema. Nauliza huwa nyongeza ya posho, ndiyo huombwa hivyo?**

"Nauliza haya kwa nia njema. Nauliza huwa nyongeza ya posho, ndiyo huombwa hivyo?"

Kutokana na mpango huo kusukwa, Waziri Kairuki, aliwataka wavae uongozi na waache kuwa wanaharakati.

Badala yake aliziagiza halmashauri nchini kushughulikia na kuyatekeleza haraka maelekezo ya Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango aliyoyatoa wakati akifungua mkutano wa siku mbili wa ALAT, Mei 29 mwaka huu.

Katika hatua nyingine, Waziri Kairuki alizitaka halmashauri kuhakikisha zinatimiza malengo ya ukusanyaji mapato na kutumia muda uliobaki kumalizika kwa mwaka wa fedha wa serikali, Juni 30 mwaka huu kutimiza makisio ya makusanyo ya ndani.

Kabla ya Waziri Kairuki kuwanang'a madiwani hao, Makamu Mwenyekiti wa ALAT Taifa, Sima Sima, alimweleza Waziri Kairuki kuwa moja ya maazimio ya mkutano huo ni pamoja na kushawishi maslahi ya madiwani kuboreshwa.



Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji Madini Tanzania (FEMATA), John Bina, akizungumza na wadau wa madini kwenye kikao cha kujadili uanzishwaji wa benki ya wachimbaji jijini Arusha jana. Wachimbaji hao, walichanga Sh. bilioni 3.6. **PICHA: GIFT THADEY**

# USAID kuongeza ushiriki sekta binafsi uhifadhi baionuai

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SHIRIKA la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), kupitia mradi wake wa USAID Tuhifadhi Maliasili, limeahidi kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika uhifadhi wa baionuai na usimamizi wa maliasili nchini.

Aidha, limepanga pia kuboresha sera, udhibiti na mazingira wezeshi kwa uhifadhi wa baionuai na usimamizi wa maliasili.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Sekta Binafsi Nchini (TPSF), Raphael Maganga, alidokeza nia hiyo ya USAID jana, alipokuwa akichangia hoja katika mdahalo wa wadau wa sekta ya umma na binafsi waliokutana suala la uhifadhi wa baionuai na usimamizi wa maliasili.

Mdahalo huo uliwashirikisha wataalamu na wadau mbalimbali wanaofanya kazi kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

"Wametuahidi kwamba wataendelea kushirikiana na serikali na TPSF kwa ajili ya uboreshaji maisha ya jamii na wanyamapori," alisema Maganga.

Kwa mujibu wa Maganga uko umuhimu wa kuweka mikakati ya pamoja ya kukuza ubia, kati ya sekta ya umma na binafsi na kukuza uwekezaji.

Mengine ni jinsi ya kupambana na wanyamapori ikiwamo kushughulikia migogoro kati ya binadamu na wanyamapori na mabadiliko ya tabianchi.

Vilevile, alisema mradi huo una nia ya kujenga uelewa kwa mashirika ya sekta binafsi (PSOs), juu ya umuhimu wa shoroba katika uhifadhi wa baionuai na maendeleo ya taifa.

Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Maurus Msuha, alipongeza ushirikiano mkubwa uliopo kati ya serikali ya Tanzania na Marekani katika kukuza uhifadhi na maeneo ya mawasiliano nchini.

"Uhifadhi lazima ulipe na ndipo tunapofanya kazi pamoja yaani, binafsi na umma, ndipo tunaweza kufikia malengo ya uhifadhi na uwekezaji,"alisema Dk. Msuha.

Kwa mujibu wa Dk. Msuha, utalii wa wanyamapori unachangia zaidi ya asilimia 80 ya utalii Tanzania Bara na unaingiza zaidi ya asilimia 25 ya fedha za kigeni na asilimia 17 ya pato la taifa.

Serikali ya Marekani, imekuwa na ushirikiano wa uhifadhi kwa miaka 60 na Tanzania na katika kipindi cha miaka mitano iliyopita USAID imewekeza zaidi ya dola za Marekani milioni 100 katika uhifadhi.



# RC awaita diaspora, wasomi kuwekeza Kagera

**Na Restuta Damian,** KAGERA

MKUU wa Mkoa wa Kagera, Fatma Mwassa, amewaomba diaspora pamoja na wasomi mbalimbali ambao ni wazawa wa mkoa huo kuungana na serikali katika kuwekeza miradi mbalimbali itakayosaidia kuinua uchumi wa mkoa na wananchi.

Alitoa wito huo jana katika kikao maalumu na viongozi wa dini na kusisitiza kuwa Mkoa wa Kagera umebahatika kuwa na watu wengi wenye uwezo wa kifedha na elimu walioko katika mikoa mingine pamoja na nje ya nchi hivyo ushirikiano wao utasaidia kuleta maendeleo.

"Tunaongoza kuwa na maprofesa wengi zaidi ya 6,000 na wasomi wengi hapa nchini, ninavyoelewa mundo wa kupanga vyeo, majukumu na madaraka hapa nchini inaangalia elimu, wasifu wako ndiyo unaangaliwa hii inatupa picha gani ni kwamba kila idara na wizara kuna diaspora ya Kagera sasa hii diaspora inasaidiaje nyumbani?" Alihoji.

Aliongeza kuwa: "Sasa niwaambie ndugu zangu huko mlipo sadaka njema inaanzia nyumbani leteni miradi mikubwa Kagera peke yetu hatuwezi."

Mchungaji Meshaki Jackob alisema kama viongozi wa dini wataonyesha ushirikiano wa kutosha kwa kiongozi huyo huku wakimwomba kushughulikia kero zinazowakumba wakulima wa mkoa huo ikiwa ni pamoja na ukosefu wa masoko ya bidhaa zinazalishwa na wakulima hao.

Alisema: "Wananchi wa mkoa huu walio wengi ni wakulima lakini bado wanakabiliwa na ukosefu wa masoko hivyo tunaomba suala hili ulivalie njuga, tusaidie kuufungua mkoa wetu kwa kuangalia ni kwa namna gani na sisi tunaweza kunufaika na hizi nchi zinazotuzunguka."

**Wananchi wa mkoa huu walio wengi ni wakulima lakini bado wanakabiliwa na ukosefu wa masoko hivyo tunaomba suala hili ulivalie njuga.**



Meneja Mawasiliano wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) Tanzania, Warren Bright (kushoto), akikagua na kukusanya taarifa kwa wasichana kuhusu mafunzo ya ufundi na ujasiriamali wanayopata katika kituo cha Masista Kahama mkoani Shinyanga mwishoni mwa wiki, ambao ni wanufaika wa Mradi wa UNFPA wa "Chaguo Langu Haki Yangu" unaofadhiliwa na nchi ya Finland, kwa lengo la kuwezesha msichana kufikia lengo lake.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Soko la kisasa Ngokolo kuzinduliwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

DIWANI wa Kata ya Ngokolo Manispaa ya Shinyanga, Victor Mkwizu, amesema ujenzi wa soko la kisasa katika kata hiyo unaendelea, kwamba unatarajiwa kukamilika Juni mwaka huu.

Alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Ngokolo Manispaa ya Shinyanga.

Mkwizu alisema serikali imekuwa ikitoa fedha nyingi za kutekelezwa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa soko la kisasa katika kata hiyo na kuwaomba wananchi waitunze miradi hiyo ili ipate kuwahudumia kwa muda mrefu.

Aidha, alisema hivi karibuni wataanza tena ujenzi wa Kituo cha Afya Ngokolo ili kuwasogezea wananchi huduma za afya kuwa karibu, pamoja na ukarabati wa miundombinu ya barabara ambazo ni korofi.

Katika hatua nyingine, alitoa wito kwa wananchi wa Ngokolo kuendelea kukemea vitendo vya ukatili, pamoja na kutoa taarifa kwenye mamlaka ili wahusika wachukuliwe hatua.

Naye Katibu wa UVCCM Wilaya ya Shinyanga Mjini, Naibu Katalambula, akizungumza kwa niaba ya Katibu wa CCM wilayani humo, alisema serikali imetoa Sh. bilioni moja kutekelezwa miradi ya maendeleo.

Baadhi ya wananchi waliomba serikali kufanya haraka ujenzi wa kituo kikubwa cha afya ili kuwawezesha kupata huduma za matibabu karibu na kuwasaidia wanawake wajawazito pamoja na watoto hususani nyakati za usiku.

**Katika mkoa huo kaguzi 50 zimefanyika na baa 31 zilikutwa na makosa ya uzalishaji kelele kwa kiwango cha juu na hakuna hoteli iliyokutwa na makosa wala kufungiwa.**

## TFS yajenga kiwanda cha kutengeneza mkaa mbadala

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wamejenga kiwanda cha kuchakata na kutengeneza nishati ya mkaa mbadala kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Kiwanda hicho kinauwezo wa kutengeneza mkaa mbadala kuanzia tani moja kwa siku na kwa wiki wanatengeneza mkaa huo mara mbili kutokana na eneo la kiwanda kuwa dogo.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake, Mhifadhi Misitu Daraja la Kwanza, Ester Josephati, juu ya namna ya kupunguza utumiaji wa misitu na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi alisema mpaka sasa wamepanda miti 438,000 maeneo mbalimbali ikiwamo zahanati, taasisi za elimu, vituo vya afya na vyanzo vya maji.

Alisema baada ya kuanzisha kiwanda hicho uvamizi wa ukataji miti ovyo katika Hifadhi ya Milima ya Mkweni umepungua kulinganisha na ilivyokuwa awali kwasababu wananchi wanajitokeza kununua mkaa huo.

Ofisa Nyuki wa TFS, Martha Machibya alisema ukataji wa misitu ovyo unakwamisha hata ufugaji wa nyuki hali ambayo imewafanya kuvitembelea vijiji vinavyozunguka Hifadhi ya Milima ya Mkweni na kuvipatia elimu ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira.

# SMCL yazindua nyumba mfano watakazopewa waathiriwa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya uchimbaji madini ya Sotta Mining Limited (SMCL) imezindua mfano wa nyumba kwa ajili ya wananchi walioathiriwa na mradi huo.

SMCL inajenga mradi wa mgodi wa dhahabu wa Nyanzaga, kwamba mradi huo upo chini ya Mpango wa Makazi ya Uhamisho (RAP), unaratibiwa na kampuni hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi na Meneja Mkuu wa SMCL, Damien Valente, mpango huo unatekelezwa kwa kuzingatia viwango vya utendaji vya IFC, na SMCL unatoa makazi hayo mbadala kwa ajili ya kaya zitakazozoathiriwa ikiwa ni pamoja na programu za kurejesha riziki.

Valente alisema mfano wa nyumba iliyozinduliwa mwishoni mwa wiki kwenye Kijiji cha Nyabila, wilayani Sengerema ni uchaguzi moja kati ya 10 za usanifu majengo ambazo zimejengwa kwa ajili ya watu watakaoathiriwa na mradi huo.

Alisema kuna kaya 725 ambazo zitaathirika kiuchumi na kimwili kutokana na kuhamishwa, kwamba kaya zipatazo 452 zitahamishwa katika sehemu ya mpango wa RAP, kila kaya italipwa fidia kwa kupewa makazi mapya.

"Kwa kuzingatia maombi ya wananchi watakaoathiriwa na mradi, mfano wa nyumba za uhamisho zilijengwa kwa kuhakikisha waathirika wanataarifa za kutosha kabla ya kuchagua aina ya fidia wanayoitaka," alisema.

Alisema hivi sasa wananchi walioathiriwa na mradi wana nafasi ya kuzikagua nyumba za mfano na wanaweza kuchagua uchaguzi za nyumba ambayo ni sawa na ukubwa wa eneo ambalo watalipoteza kwenye makazi yao ya sasa kama sehemu ya mchakato wa uhamisho.

Valente alisema baada ya mchakato wa ukaguzi utakapotimia SMCL itatoa nyumba hiyo ambayo itatumika kama ofisi ya Baraza la Kijiji cha Nyabila.

Ukurasa 13




**Tatizo bangi, mirungi linavyosumbua ukanda mpakani Namanga, Longido**



**KUELEKEA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI... Vita vya plastiki vinavyokamata ajenda, wadau pia wakiwa na yao**

Ukurasa 12

## KUELEKEA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI...

# Tangu hatua ya kwanza, Rais akiongoza Watanzania kuelekea mazingira bora

**Na Mwandishi Wetu**

WIKI ya Mazingira imeanza. Ni suala la dunia, pia kitaifa kwa ujumla, ikianzisha uwajibikaji moja kwa moja kwa mkuu wa nchi hadi umma wa Watanzania wote.

Rais Dk, Samia Suluhu Hassan anaendelea kuwa mbia muhimu kitaifa katika vita vya kukabili utunzaji mazingira kwa zaidi ya muongo mmoja sasa, tangu akiwa waziri anayewajibika na mazingira.

Hata baadaye akiwa Makamu wa Rais zaidi ya miaka saba sasa, akabaki katika ofisi iliyokabidhiwa kisheria na kisera, jukumu kuu la kulinda mazingira, kabla ya kubeba jukumu la kusimamia taifa, akiwa rais wa nchi zaidi ya miaka miwili sasa. Hiyo inamtwika wasifu kuwa mwanamazingira.

Wakati akikarabia kutimu mwaka mmoja wa urais, Februari mwaka jana, Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 ilizinduliwa nchini, ambayo kihistoria mzizi wa maandalizi yake una 'mkono wake', Rais Dk. Samia tangu zama alipokuwa Makamu wa Rais kwa miaka sita, amehusika nayo moja kwa moja kuiandaa.

Miezi mitano baada ya kuzinduliwa sera hiyo, mnamo Julai 12 mwaka jana, Rais Dk. Samia akaelekeza haja ya kuwapo jitihada na ushirikiano katika kufanikisha utunzaji mazingira katika sifa pana, barani Afrika.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika zama akiwa Makamu wa Rais, akishiriki kuzoa taka na baadhi ya wananchi wakazi wa eneo lake la Oysterbay, katika Barabara ya Karume, Dar es Salaam, kwenye maadhimisho ya miaka 54 ya Uhuru wa Tanzania. **PICHA: MTANDAO.**

"Niwaombe sana kuendelea kushirikiana na serikali kama mnavyofanya sasa, katika kuendeleza mapambano ya uharibifu wa mazingira..." akatamka Rais Dk. Samia, Julai mwaka jana, alipohutubia Mkutano wa Shirikisho la Mabaraza ya Maaskofu Katoliki Afrika Mashariki na Kati (AMECEA) mjini Dar es Salaam,

Anataja magonjwa mengi ya mlipuko hutokana na uchafu unaosababishwa na kutotunzwa mazingira, huku akiitaka sekta binafsi kuiga mfano wa viongozi wa dini, wanaokuwa mstari wa mbele kwenye juhudi za kutunza mazingira.

Kimsingi, AMECEA ni mkutano unaoandaliwa na viongozi wa Kanisa Katoliki kutoka nchini za Eritrea, Ethiopia, Malawi, Kenya, Sudan, Sudan Kusini, Tanzania, Uganda, na Zambia.

Ni dhana ambayo Rais Dk. Samia ana msisitizo wake huku akirejea maandiko ya kiimani kwamba, ujumbe wa kutunza mazingira ni muhimu katika kipindi kilichopo dunia inakabiliwa na athari nyingi zitokanazo na uharibifu wa misitu, madhara yanamfikia binadamu.

Wakati akizungumza kwenye hafla ya ufungaji lango litakaloruhusu maji kuanza kujaa kwenye Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Nyerere (JNHPP), Desemba mwaka jana, Rais Dk. Samia Suluhu akatoa angalizo kutetea mazingira na vyanzo vya maji.

Akasema, hakuna aliye mkubwa zaidi ya sheria za nchi, akiagiza kuchukuliwa hatua dhidi ya wote wanaodaiwa kutunishia misuli wakuu wa wilaya na mikoa kuingiza mifugo kwenye ardhi oevu.

Rais Samia akasema manufaa ya bwawa hilo yataonekana endapo vyanzo vinavyopeleka maji vitatunzwa, huku Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiunga mkono kwa maelekezo ya kuondolewa mifugo yote kwenye Bonde la lhefu, huku akiwataka wakuu wa mikoa kusimamia kikamilifu na uwezo wa vijiji uangaliwe kabla ya kupeleka mifugo.

**MAKAMU RAIS**

Ikiwa ni hoja ya kitaifa ya Serikali ya Awamu ya Sita, katika uzinduzi wa Sera ya Mazingira Februari mwaka jana, Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango anamuunga mkono Rais Dk. Samia, akisisitiza ni jukumu la lazima kuhifadhi mazingira kunakojumuisha; upandaji miti, kupendezesha miji, kulinda vyanzo vya maji, misitu, usafi wa makazi, penye biashara, viwandani na sokoni.

Hapo Dk Mpango anaelekeza kuwa ni jukumu la viongozi wote kuanzia ngazi vijiji hadi mikoani, inayokuwa sehemu ya kipimo chao cha utekelezaji majukumu wanayopewa.

Katika hilo, miezi kadhaa baadaye, Julai mwaka jana, Rais Dk. Samia akaweka mkazo kwa wito wake, akinukuu kifungu cha maandiko ya kiimani, inayosisitiza haja ya kulindwa maliasili.

Mwaka huo uliopita kaulimbiu ya mwaka jana iligusa kujadili umuhimu wa mazingira na kuwahamasisha wafuasi wa kiimani kuyatunza.

Kumrejea Makamu wa Rais, kazi ya kulinda na kuhifadhi mazingira inagusa ulazima wenye mtazamo endelevu kwenye jicho la kulinda

Inaendelea Uk. 14

MAZINGIRA

## KUELEKEA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI...

# Vita vya plastiki vinavyokamata ajenda, wadau pia wakiwa na yao



Hali iliyoko katika ufukwe Rainbow, Mbezi Beach, , Dar es Salaam, uliojaa taka za plastiki zilizotumiwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU..**

**Na Jenifer Gilla**

TAREHE 5 ya mwezi Juni, Tanzania inaadhimisha miaka 50 ya Siku ya Mazingira Duniani, pale Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP), lilipotaja kaulimbiu kutafuta suluhisho la kutokomeza taka za plastiki, zinazoonekana kuwa kero.

Ni utaratibu unaofanyika kila mwaka tarehe kama hiyo, lakini mwaka huu UNEP inaeleza lengo kuu ni kuikumbusha jamii kuwa ina mchango mkubwa katika uchafuzi wa mazingira, kwa kutumia vifaa vya plastiki, pia kwa serikali na aina ya biashara ndivyo vitaamua kukuza au kutokomeza tatizo hili.

Tanzania ni moja ya nchi zinazokabiliana na changamoto ya uwapo wa wingi wa taka za plastiki zinazozagaa mitaani na pembezoni mwa bahari, licha ya juhudi kubwa zinazofanywa na serikali na mamlaka za mazingira kutokomeza.

Kuna juhudi zinafanywa na wadau wa mazingira wanaoingia mitaani kuhamasisha jamii kuondoa taka za plastiki katika mazingira yao, ikiwa ni kuunga mkono juhudi za serikali kutokomeza uzagaaji wake. Hata hivyo, visiwani Zanzibar, kuna mafanikio makubwa yamefikiwa, kukabili shida hiyo ya plastiki.

**KUTOKA TAASISI**

Mkurugenzi wa Taasisi ya Mikakati ya Maendeleo Endelevu (TSDI), Fredy Kwezi, ni mmoja wa wadau hao anayesema kila mwezi wanahamasisha jamii kusafisha fukwe za Bahari ili kuweka mazingira hayo safi.

Anasema ni mkakati waliouanzisha miaka mitatu iliyopita, baada ya kuona hali ya fukwe kuwa mbaya, akitoa mfano fukwe za 'Rainbow' iliyoko Mbezi Beach, Dar es Salaam, zilikuwa zimetapakaa taka za plastiki kiasi cha kupoteza mvuto kwa wanaopenda kutelembelea, hasa wageni.

Kwezi anasema, kila walipokuwa wakienda kusafisha fukwe hizo wanakusanya wastani wa viroba 30 vya taka za plastiki na kila wanaporudi wanakuta taka zikiwa zimeongezeka, jambo linaloonyesha watu wanaendelea kutupa kila siku.

"Ilibidi tuanze kazi ya kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kutunza yale mazingira na kuchagua viongozi watakaosimamia usafi, angalau sasa hivi uchafuzi sio mkubwa na watu sasa wanaonekana kufurahia fukwe na biashara ndogo ndogo zinafanyika bila kuchafua mazingira," anafafanua.

Mwingine, Mkurugenzi wa Kampuni ya Libe Greed Innovation, Liberatha Kawamala, inayokusanya plastiki zilizotumika na kutengeneza mapambo ya nyumbani ikiwamo maua ya plastiki, bustani ya plastiki na 'flakes'.

Kupitia ubunifu huo, Liberatha anapatia pesa kwa kuuza bidhaa hizo sehemu mbalimbali nchini, hali inayochangia kumwongezea kipato, pia inapunguza taka za plastiki zinazozagaa mitaani.

Liberatha anasema, taasisi inatoa elimu kwa waokota taka namna nzuri ya kukusanya na kujipatia kipato, hali iliyoongeza idadi ya waokota taka za plastiki.

**KUTOKA NEMC**

Kwa upande, mwigine kuna Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), ambalo linafanya kazi ya kuondoa mifuko ya plastiki isiyo na viwango, ilikuwa ikiishia kuzagaa mitaani na kuharibu taswira ya mazingira.

Hadi sasa NEMC, imekuwa ikitembelea viwanda vinavyozalisha vifungashio hivyo na kuhakikisha vinazalishwa vyenye ubora unaotakiwa pamoja hali iliyochangia kutokomeza taka za aina hiyo.

Pia, chombo hicho kimekuwa kikitoa elimu kwa jamii, kuhusu madhara ya taka za plastiki kiafya na kimazingira ikiwamo kutoa sumu inayoweza kusababisha kansa kwa binadamu na pia kuchafua mazingira.

Ofisa Mazingira wa NEMC, Kulthum Shushu, anasema baraza hilo sasa lipo katika mchakato wa kuandaa teknolojia ya kuteketeza taka zinazoonekana kero, hasa pampasi zinazozagaa kila sehemu nchini.

"Udhibiti wa hizi taka ngumu upo katika ngazi ya halmashauri, lakini tunashirikiana nao kwa kutoa elimu kwa jamii juu ya madhara ya kuzagaa taka hizo kwa afya na mazingira. Pia, tunahakikisha plastiki zinazozalishwa au kuingizwa nchini zina viwango vinavyohitajika," anasema.

**NINI KIFANYIKE?**

Mtaalamu wa Mabadiliko ya Tabianchi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. Pius Yanda, anasema ingawa Tanzania imepiga hatua kutokomeza taka hizo kwa kuboresha sera na sheria, nguvu inahitajika kuongezwa katika utekelezaji wa sera hizo.

"Kwanza Tanzania imepiga hatua kubwa, nchi nyingi zinasifu hatua iliyofikia ya kuondoa mifuko ya plastiki isiyokuwa na viwango. Hii yote imetokana na kubadilishwa kwa sera na kuzifanyia kazi matakwa yake" anasifu Prof. Yanda.

Anashauri mamlaka zinazosimamia sera na sheria kutumia njia na nguvu iliyotumika kumaliza tatizo la mifuko ya plastiki isiyo na viwango, sasa kushughulikia chupa za plastiki, vifungashio na taka kero kwa mazingira.

Msomi huyo anadems, wakati wanazuia kuzaga huko, watoe bidhaa mbadala zinaziweza kupatikana kwa bei nafuu, akitoa mfano wa mifuko ya karatasi ambayo kwa sasa ni mbadala mkuu wa mifuko ya plastiki iliyopigwa marufuku.

Mtaalamu huyo wa mazingira, anapendekeza kuwapo teknolojia ya kutengeneza mifuko, itkayotumika kwa muda mrefu, ili kupunguzwa utupaji mifuko holela .

Mkurugenzi wa Shirika la Utu na Mazingira, Sarah Pima, anasema kuna haja ya kupunguza matumizi ya vifungashio vya chakula na kurudi katika utaratibu wa zamani wa kutumia udongo, kwa kuwa taka hizo zinaongoza kutupwa ovyo.

"Zile wanazosema 'take away' zinaishia kutupwa ovyo, ukienda baharini unakuta pembezoni kumejaa sahani na vikombe vya 'take away' na 'pempasi'. Hili ni tatizo kubwa sana , nafikiri hata kwenye 'pempasi' turudi kwenye utaratibu wa nepi kwa sababu taka hii ni kero kubwa" anasema Sarah.

Ripoti mpya ya Shirika la Umoja wa Mataifa kla Mazingira (UNEP), inaeleza kuwa uchafuzi wa plastiki unaweza kupunguzwa kwa asilimia 80 kufikia mwaka 2024, iwapo nchi na mashirika zikiweka sera thabiti na mabadiliko ya masoko, kwa kutumia teknolojia iliyopo.

Inapendekeza mabadiliko matatu kwenye mfumo wa biashara ambayo ni 'isha, kutumia tena' ikiwa na maana kutengeneza bidhaa zinaweza kutumika kila mara, mfano wa chupa kubwa za lita 13, zinawekea maji ya kunywa ambazo zikiisha maji, mteja anarudisha dukani na kupewa nyingine yenye maji.

Njia ya pili anataja ni kuchakata. Ripoti hiyo inasema, hilo linawezekana, iwapo serikali itaondoa ruzuku kwa baadhi ya mahitaji ya utengenzaji, kutekeleza yaliyomo kwenye mwongozo wa kukuza uchakataji, na hatua nyinginezo kuongeza kiwango cha plastiki inayoweza kuchakatwa kutoka asilimia 21 hadi asilimia 50

Njia ya tatu inatajwa na UNEP, ni kubadilisha kwa uangalifu bidhaa za mifuko ya plastiki na vitu vya plastiki vya kupakia chakula, kwa bidhaa zilizotengenezwa kutoka kwa nyenzo mbadala kama vile makaratasi au vitu vinavyoweza kuoza, plastiki iliyochakatwa. Hiyo inaweza kupunguza asilimia 17 ya ziada ya uchafuzi wa plastiki.

MAZINGIRA

# Tatizo bangi, mirungi linavyosumbua ukanda mpakani Namanga, Longido

## • Kinamama, watoto wakala wakuu duniani




**Na Zanura Mollel**

DAWA za kulevya ni kemikali ambazo zikiingia mwilini, huathiri ubongo wa mtumiaji na kumsababishia matendo, hisia, fikra na muonekano tofauti na matarajio ya jamii.

Kemikali hizo zinatokana na mimea, pia madini ambayo yana mahitaji mengine kwa mwanadamu. Huingia mwilini kwa njia kuu tatu; kunywa au kula, kuvuta na kujidunga sindano.

Zipo dawa za kulevya zilizoruhusiwa kisheria kama tumbaku na pombe na kwa matumizi ya hospitali kuna Valium, pethedine, morphine. Pia, zisizoruhusiwa ni kama bangi, mirungi, cocaine, heroin na mandrax.

Dawa za kulevya sasa ni janga kubwa duniani, watu wengi wameathirika wa jinsia zote, vijana na wazee.

Nchini, katika nafasi ya pekee kati baadhi ya maeneo, kuna shida ya bangi na mirungi zikitawala, ikiwamo mkoani Arusha.

Vijana ni kundi kubwa linalokabiliwa na kadhia ya matumizi na usafirishaji wake, hasa wanaoanzia umri miaka 15 wakichochewa na mitandao ya kijamii, huku ukiwapo upande hasi dhidi ya kukua diplomasia ya uchumi duniani.

Dawa za kulevya ni sehemu ya matukio ya kihalifu duniani, usafirishaji wake ukihusisha magenge ya kihalifu kimataifa, kwa kushirikiana na makundi ndani ya nchi.

Kwa sasa, vijana na wanawake ndio wameibuka kutumika katika sana kusafirisha dawa hizo, kutokana na hali ngumu za kiuchumi zinazowakabili, wanarubuniwa kuwa sehemu hya nyendo hizo.

### MPAKANI NAMANGA.

Hiyo ni sehemu iliyoko wilayani Longido mkoani Arusha na Kajado nchini Kenya, miongoni mwa mipaka inayounganisha nchi hizo na mataifa pacha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki(EAC) .

Kwa usafirishaji na usambazi wa dawa za kulevya, Mkurugenzi wa Kinga na Tiba wa Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya (DCEA), Dk.Peter Mfisi, anayetamka yuko katika operesheni mkoani Arusha, anakiri changamoto ya bangi na mirungi imetawala mpakani Namanga.

Ofisa Uhamiaji mkoani Arusha (jina tunalo), anaifafanulia Nipashe, akinena: "Mpaka huo ni mkubwa na una vipenyo vingi sana vya kuingia Tanzania na Kenya na baadhi ya vipenyo hutumia usafiri wa magari, pikipiki na miguu, "

"Kuna baadhi ya maeneo nchini yaliyopo pembezoni na nchi ya Kenya, hufanya biashara kwa thamani ya fedha ya nchi hiyo, ikiwamo kijiji cha Wosiwosi kilichopo Kata ya Gelailumbwa Tarafa ya Ketumbeine wilayani Longido."

Ukubwa wa biashara hiyo Arusha, pia unatajwa kuchangiwa na uhalisia, majirani Kenya wamehalalisha kisheria mihadarati, tofauti na Tanzania ambayo ni jinai.

Hata hivyo, ukubwa wa biashara hiyo ya bangi na mirungi, inatajwa kusukuma kasi ya kulimwa katika nchi zote jirani; Kenya na Tanzania.

Ofisa Uhamiaji wa mkoani Arusha, anasema nchini Tanzania, serikali kwa kushirikiana na raia, inajitahidi kupambana, kudhibiti na kukemea matumizi ya dawa za kulevya na haijashindwa kufanikisha vita hivyo vigumu, mahsusi mipakani .

Anataja kikwazo kikuu katika vita hivyo, ni uhalali uliopo katika upande wa nchi jirani, hata kuteka nyendo za wakazi wengi waliopo jirani, pia watendaji wa kiserikali nchini katika maeneo hayo, kushirikishwa katika njama za kusafirisha dawa, hata zikaingizwa nchini, pia kuvushwa nje.

### LANGO LA USHUHUDA

Mchungaji, Obadi Kiango, katika Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, mpakani Namanga, Juni mwaka jana, akasema watoto nchini wako hatarini kwa matumizi ya dawa za kulevya, pia wazazi na walezi.

Anashauri wamiliki wa nyumba zinazofanya biashara ya bangi, wachukuliwe hatua kisheria, akitumia mfano vijana waliomaliza kidato cha nne wameadimika kanisani, wengi wamekimbilia biashara za bangi na mihadarati.

Ni simulizi inayoendelezwa na mkazi wa Buguruni, jirani na mpaka wa Namanga, akitoa ushuhuda kumuona mtoto mwenye umri wastani miaka 10, akiwa amebeba mfuko ambao ndani yake kulikuwamo galoni na akamfuatilia.

Anaendelea: "Mtoto yule alikuwa akielekea upande wa Kenya, kabla hajaingia Kenya nilimkamata na kumuuliza umebeba nini? Mtoto yule alionyesha hofu, lakini mwisho wa siku nilifungua mfuko ule na kukuta alikua amebebeshwa bangi. Nikamuuliza umetoa wapi na unapeleka wapi?

"Akadai alitumwa na baba yake mzazi apeleke kwa mama mmoja upande wa Kenya. Nilimshika mkono nikamwambia nipeleke hadi nyumbani kwenu,tulielekea na tulipofika baada ya baba wa mtoto kutuona, alikimbia na kumuacha mwanaye..."

Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya nchini (DCEA), Aretas Lyimo. akiwa mkoani Mtwara kwenye uwashaji Mwenge wa Uhuru 2023, anataja mkakati wao ni kuhakikisha Tanzania inadhibiti utumiaji dawa hizo.

Hapo anatoa angalizo wa ujio wa msako nchi nzima, akiwaomba viongozi wa dini kutumia majukwaa yao kuelimisha jamii ubaya wa dawa za kulevya.

### RIPOTI YA DUNIA.

Mkurugenzi Mtendaji wa Ofisi ya Umoja wa Mataifa inayohusika na Dawa na Uhalifu - UNODC, Ghada Waly, akitoa ripoti anasema idadi ya wanaotumia mihadarati duniani inaongezeka , mwaka 2020 kulikuwapo watu milioni 275 duniani, ikiwa ni ongezeko la asilimia 22.

"Zaidi ya watu milioni 36 wamepata shida kutokana na utumiaji wa dawa za kulevya, dawa hizi zimesababisha vifo vya takriban watu nusu milioni kwa mwaka 2019" anasema Mkurugenzi Mtendaji huyo wa UNODC.

Vilevile, Ripoti ya Mwaka 2022, inatamka watu milioni 284 wenye umri wa miaka 15 hadi 64 walitumia dawa hizo duniani mnamo mwaka 2020, ikiwa ni ongezeko la asilimia 26 katika muongo uliopita.

"Vijana wanatumia dawa nyingi zaidi na viwango vya matumizi leo katika nchi nyingi, ni vya juu kuliko kizazi kilichopita," inatamka ripoti hiyo.

Barani Afrika na Amerika Kusini, watu wenye umri chini ya miaka 35, wengi wanaotibiwa matatizo ya kutumia dawa za kulevya, inaeleza ." Imeeleza taarifa ya UNODC iliyotolewa kwa vyombo vya habari jijini Vienna, Austria.

Ni ripoti inayokadiria watu milioni 11.2 duniani, walikuwa wakijidunga dawa ya kulevya. Takribnai nusu yao wanaishi na ugonjwa wa Hepatitis C ni ugonjwa unaosababishwa na virusi kupitia damu, ukilifanya ini livimbe.

Pia, inaelezwa watu milioni 1.4 wanaishi na Virusi vya Ukimwi, huku wengine milioni 1.2 wana magonjwa yote mawili.

### UZALISHAJI 'UNGA'

Utengenezaji dawa za kulevya aina ya Cocaine duniani, unatajwa kuwa juu zaidi, mnamo mwaka 2020, ulikuwa kwa asilimia 11 kutoka mwaka 2019, tofauti hiyo ni tani 1,982.

Vilevile inatajwa ukamataji Cocaine, nao uliongezeka kwa wakati huo, ikirejewa mfano asilimia 90 iliyokamatwa duniani mwaka 2021 ilikuwa inasafirishwa, hasa katika meli baharini. Takwimu za ukamataji zinataja zaidi Amerika Kaskazini na Ulaya, huku bara Afrika na Asia, viwango vinaongezeka.

Pia, utumiaji bangi unatajwa kushamiri Afrika na Amerika Kusini, huku Ulaya ya Mashariki, pia Bara Asia ya Kusini, Mashariki na Kati, wamezama zaidi katika dawa nyinginezo za kulevya, maarufu 'unga'.

AFYA

## VITA VYA HEDHI KWA MABINTI

# Wadau wachachamaa na darasa, wakifuta usiri kuonyesha mchango wa baba uliko

**Na Pilly Kigome**

INAPOTAJWA hedhi, inaangukia kuwa suala mtambuka, haimhusu mwanamke peke yake, pia mwanaume. Hapo hoja ni pale penye haja ya kuleta matokeo chanya na kuondoa changamoto zilizopo kwa wasichana na wanawake kuanzia ngazi ya familia.

Awali ilikaririwa masuala ya hedhi yanawahusu wanawake pekee, wanaume wakiwekwa kando, kutokana na dhana tofauti inayotawala jamii, ikiwamo mila, utamaduni, miiko ya makabila na hata dini.

Sasa yamekuja mageuzi, elimu hiyo ya hedhi inawaangukia pia wazazi, ili kuwezesha kuondolewa changamoto zinazojitokeza au kuzimaliza kabisa.

Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), imeliona hilo na kuanza kupaza sauti ya kutoa elimu kwa wanaume kupitia semina zao za jinsia na maendeleo, lengo ni kuwawezesha wanaume.

Na hapo ni kuondoa dhana ya suala hedhi sio jukumu lao na kuwaachia wazazi wakike pekee.

Kurejea Siku ya Hedhi Duniani ya Mei 28, TGNP imepaza sauti kuwafikia kinababa ikiwajengea uwezo kupitia elimu hiyo ili wachukue hatua, ikiwamo kubeba majukumu wanayodhani hayawahusu.

Kaulimbiu ya maadhimisho ya mwaka huu inasema: "Hedhi ni tunu kwa wasichana na wanawake, tuwawezeshe."

Mtazamo unaotawala sasa unafika mbali, kutaka kufikiwa kitaifa kupitia halmashauri zake kote nchini, kutengwe bajeti maalum kuhusiana na suala hilo,



Wanafunzi wa shule ya sekondari, wakifurahia jambo pamoja na muwezeshaji wao, baada ya kupatiwa taulo za kike shuleni. **PICHA: MTANDAO.**

katika maeneo muhimu ikiwamo shuleni, nyumba za ibada, sokoni na vituo vya mabasi ya safari za mbali, ili kuondoa changamoto zinazowakabili wasichana na wanawake, wanapokutwa na hali hiyo.

Tafiti nyingi nchini zinagundua matokeo mabaya kwa Watoto wa kike hasa vijijini kutokana na changamoto zinazowakabili pindi wafikiapo kipindi hicho.

Mshauri Mwandamizi wa Afya ya Uzazi kutoka Jukwaa la Hedhi Tanzania, pia Mkurugenzi kutoka asasi Tanzania Boys and Mens Ambassador (TBMA), Dk. Katanta Simwanza, anasema watoto wa kike waishio nje na mijini, wamekuwa wakikabiliwa na changamoto nyingi kuliko wa mijini, katika hali hiyo.

Anafafanua ni hali inayochangiwa pia kutokana na usiri uliowekwa kwa wanaume, kuhusiana na masuala ya hedhi ikiwamo wazazi wa kike kutowajibika kwa watoto wao, wafikapo kipindi hicho.

Hivyo inaelezwa, mabinti wamekuwa wakijitafutia vifaa vya hedhi na kusababisha baadhi yao kushiriki mapenzi ya utotoni, ikiwamo kupata mimba za utotoni, kupata maambukizi katika njia za uzazi.

Anasema, wamekuwa wakikumbana na vitendo vya ukatili na hata kupata ulemavu wakati wanajaribu kujitafutia vifaa hedhi, ili wajisitiri kutokana na kurubuniwa.

Sababu za kiuchumi zikiwamo ukosefu wa elimu kwa watoto hao kukiwekwa na mipaka kutoka kwa wazazi, imekuwa ikiwagharimu watoto, kwa kukutana na misukosuko, ambayo mwisho wake inawakatisha ndoto za baadae.

Inadaiwa, kuna wanaume wamekuwa wakiwasababishia athari kubwa watoto wa kike, ikiwamo mimba za utotoni, magonjwa na maambukizi mapema kwa kukosa kifaa cha hedhi.

### HATARI YA MIMBA

Mabadiliko ya hali ya hewa, ni changamoto nyingine inayosababisha mimba za utotoni kwa kufuata maji umbali mrefu.

Ukosefu wa vifaa hedhi na ukosefu wa elimu kwa wasichana, imekuwa ikiwagharimu na kuna tafiti zilizogundua kujihifadhi kwa kutumia makaratasi, majani na hata michanga pindi wafikiwapo na hali hizo kwa ukosefu wa wazazi kukosa kuwatimizia vifaa hivyo.

Tafiti zimegundua vitendo hivyo vya kujihifadhi kwa kutumia vifaa ambavyo si sahihi, kunaleta madhara makubwa ikiwemo na kupata maambukizi mapema katika njia ya uzazi.

### KAULI YA KITAFITI

Mtaalamu wa masuala ya maji na usafi wa mazingira, pia muwezeshaji wa elimu hedhi kikanda na kitaifa, Dhahia Mbaga, miundombinu rafiki kwa wasichana na wanawake kutaleta tija kubwa sana mijini na vijijini kwani wataweza kushiriki vyema shughuli zao za kimaendeleo na hata kiuchumi.

Mbaga anaiambia Nipashe kuwa, wasichana na wanawake wanatakiwa wawekewe mazingira rafiki kuanzia ngazi ya familia na hata taifa kwani hedhi ndio taifa lenyewe.

Anashauri wanaume washirikishwe kwa kiasi kikubwa kuanzia ngazi ya familia na kutokuwekewa mipaka na Watoto wao wa kike katika suala zima la hedhi kwani kushirikishwa kwao kutaweza kuwawekea mazingira rafiki ikiwemo maji, choo chenye usiri, na hata sabuni.

Anafafanua wasichana wanapokosa mazingira wezeshi ya vifaa hedhi na kutumia mbadala duni, kunaleta madhara makubwa ikiwamo magonjwa ya maambukizi. Baadhi ya wanaume waliongea na Nipashe, wanaiambia kuwa ni wakati wao kutenga bajeti za kuhusiana na hedhi kwani kufanya hivyo kutarahisisha kukwepa changamoto za Watoto wa kike.

Edson Ramadhan mkazi wa Manzese, Dar es Salaam, anataja mfano hai, kwamba aliwahi kuona binti mwanafunzi, aliyekaribia kufikwa na hali hiyo, anaenda kumueleza mpenzi wake wa kiume kwa kuficha aibu hiyo kwa mzazi wake wa kiume, hali anayoitaja ya kusikitisha.

Anasema, pale elimu ya hedhi ingewafikia wazazi, mabinti wangewawasilishia hoja hiyo moja kwa moja.

Ramadhani anasema, ni hali inayojitokeza na kuna wakati inachangiwa utamaduni wa Kiafrika kutenganishwa na watoto wa kike, hali inayowafanya watoto kuwaogopa.

## TANGU HATUA YA KWANZA, RAIS AKIONGOZA WATANZANIA KUELEKEA MAZINGIRA BORA

Inatoka Uk. 11

vyanzo vya maji, misitu, upandaji miti, kupendezesha miji, usafi kwenye makazi na biashara, viwandani na sokoni

Anawasilisha wito unaowagusa viongozi wote kuanzia ngazi ya vijiji hadi mikoa, kwamba wanapaswa kusimamia uhifadhi wa mazingira, huku ukibaki kuwa kipimo cha utekelezaji wa majukumu yao.

Dk. Mpango anasisitiza kwamba, sasa ni wakati muafaka wa kuondoa nadharia katika uhifadhi mazingira, kukihitajika kazi ya ziada zinatazotoa matokeo chanya katika eneo hilo.

Anafafanua haja ya kuwapo sheria ndogo za kuhifadhi mazingira katika ngazi ya halmashauri, zinapaswa kusimamiwa, ikiendana na tozo za faini katika kukomesha waharibifu wa mazingira.

Makamu wa Rais, anasema baadhi ya viongozi nchini kwa maslahi binafsi, wanachangia uharibifu wa mazingira na ametoa maagizo matano katika kusimamia udhibiti wa uharibifu huo.

Katika hali yenye unasaba na mazingira, anaiagiza Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kutii agizo la Rais Dk. Samia, ikiendelea na mikakati ya kuchangia sekta hiyo kukuza uchumi (mwaka jana), akisema wakati huo mwaka jana, akailaumu sekta ya Mifugo, haikuwa na mikakati thabiti kukabili adha ya mazingira kwa ufasaha.

Ilikuwa katika ufafanuzi wake kuhusu uharibifu wa mtiririko wa maji ya mto katika Bonde la Usangu, wilayani Mbarali unaofanywa na wanaotajwa 'wazito' yeye akiahidi kuchukua hatua, akilenga kulinda Mto Ruaha Mkuu unaopita mahali hapo.

"Chukueni hatua sasa, chukueni hatua leo. Bomoeni kwa gharama zao, wale wenye vibali ambao pia wameweka vizuizi, nataka kuviona mniletee," akatamka kwenye mkutano unaohusu mazingira, mwaka jana.

Pia, akaagiza kupelekwa tathmini ya matumizi ya ardhi, ili kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira nchini, pia kukamilishwa haraka kwa kazi ya kuweka mipaka ya Ruaha.

Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi, Godwell Ole Meing'ataki, akasema Bonde la Ihefu limevamiwa na kwa siku 130 (mwaka jana) halitiririshi maji kwenda katika vyanzo vya kufua umeme na uzalishaji, akituhumu kuwapo majengo yaliyovamia ukanda wa mtiririko wa maji. Hata hivyo ni mada tata kwa sasa, wananchi wakazi wao nao wakiwa na malalamiko yao kinzani, aina ya msuguano ambao sasa unafanyiwa kazi katika ngazi ya bunge, chini ya usimamizi wa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Dk Mpango anahitimisha hoja kwa wito kuwakumbusha Watanzania kuchangamkia soko jipya aliloanzisha Rais Dk. Samia, la kutunza mazingira kwa kufanya biashara ya hewa ukaa, akitoa mfano wa kinachoendelea katika Wilaya ya Tanganyika, mkoani Katavi, umma ukivuna fedha.



## HABARI DODOMA

# Mikoa saba kunufaika na miradi ufugaji nyuki

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MRADI wa kuboresha mnyororo wa thamani wa ufugaji nyuki (BEVAC) umepanga kuwafikia wananchi 10,000 katika mikoa saba ili kuongeza kiwango cha uzalishaji asali nchini, kufikia asilimia 20 ya uuzaji wa bidhaa hiyo katika soko la nje.

Meneja wa mradi huo unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) na kutekelezwa na Shirika la Maendeleo la Ubeligij, Martin Mgallah, akizungumza katika mahojiano na Nipasje juzi alisema tangu mradi huo umeanza mwaka 2021 umeshawafikia wafugaji nyuki zaidi ya 3,000.

Alisema mahitaji ya asali ya Tanzania katika soko la nje ni makubwa lakini kiwango kinachosambazwa ni asilimia nne tu ambacho kimekuwa kikiuzwa katika nchi za EU, America na Urabuni na hivi sasa limepatikana soko jipya la asali nchi Poland.

Mgallah alisema siYo kwamba Tanzania haina uwezo wa kuzalisha asali ya kutosha bali tatizo asali nyingi inapotea kwa sababu ya kukosa ubora.

"Masoko ya nje yana viwango vinavyotakiwa hivyo kinachofanywa na BEVAC ni kuwafundisha wafugaji nyuki ili asali nyingi isipotee iweze kuingia kweye soko kubwa ambalo lina tija na litaweza kuingizia nchi fedha za kigeni," alisema.

Mgallah alisema mradi huu ambao ni wa miaka minne ulianzishwa kutokana na serikali kuona sekta ya nyuki haina msukumo mkubwa wakati asali ina soko kubwa nje lakini asali ya Tanzania ilikuwa inakosa ubora kwasababu wafugaji walikuwa wakifuga nyuki kwa njia za kienyeji na hivyo asali wanayovuna inakuwa haina viwango vya kimataifa.

"Tanzania ni nchi ya pili barani Afrika kwa kuzalisha asali ya kwanza ni Ethiopia na asali ya Tanzania iliyobora inatoka katika misitu ambayo ni asili, hivyo masoko ya Ulaya yanapenda sana asali ya Tanzania hivyo kuanzishwa kwa mradi wa BEVAC ilikuwa ndio suluhisho la kutatua changamoto ya asali," alisema.

Mgallah alisema BEVAC imekuwa ikiwaunganisha wazalishaji wa asali wa mikoa ya Singida, Kigoma, Shinyanga, Katavi, Tabora, Pemba Kusini na Pemba Kaskazini ambako mradi huo unatekelezwa na masoko ya ndani na nje kwa kuwawezesha ili kuyafikia masoko hayo.

# Maofisa Wizara Mambo ya Ndani watakiwa kutolala usingizi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Kaspar Mmuya, amewataka wasemaji, maofisa habari wa wizara hiyo pamoja na vyombo vya usalama kutoa taarifa ya matukio yanayotokea mapema ili kuondoa mkanganyiko ambao umekuwa ukijitokeza katika jamii.

Alitoa agizo hilo juzi alipokuwa akifungua mkutano wa mwaka na mafunzo kwa wasemaji, maofisa habari wa wizara na vyombo vya usalama uliofanyika katika ukumbi wa makao makuu ya Jeshi la Magereza jijini hapa.

Alisema wasemaji na maofisa habari wa wizara hiyo pamoja na vyombo vyake vya usalama wanapaswa kutekeleza majukumu yao ya kuhabarisha umma kwa kila tukio linalotokea.

"Siku hiyo teknolojia imekuwa sana kila mtu ni mwanahabari hivyo mnapaswa nyie kuwa wa kwanza kutoa taarifa za matukio mbalimbali ambayo yamekuwa yakitokea kabla ya watu wengine ambao wanaweza kutoa taarifa zisizokuwa na ukweli na kuleta taharuki katika jamii,"alisema.

**Pale ofisini ninayo malalamiko ya watu kustafu wakiwa na vyeo vikubwa lakini mishara ipo chini hivyo wanaopandishwa vyeo lazima na mishara yao isome kulingana na vyeo vyao na nitafuatilia hili.**

Alisema mara nyingi kumekuwepo na tabia ya watu kuweka taarifa zinazohusu matukio mbalimbali kwenye mitandao ya kijamii ambazo hazina ukweli wakati wenye jukumu hilo ambao ni maofisa habari wa wizara hiyo wanashindwa kutekeleza majukumu yao.

"Mnapaswa kubadilika kwenda na wakati kwani nyie ndiyo wenye dhamana hii mnapochelewa kutoa ufafanuzi wa jambo fulani linalohusu taasisi zenu watu wengine wanafanya hivyo lakini kinyume na maadili ya uandishi wa habari kwa 'kupost' vitu ambavyo havizingatii maadili,"alisema.

Kadhalika, aliwataka wakuu wa vitengo vya habari katika wizara hiyo na vyombo vya usalama kuhakikisha kuwa wanazitumia nafasi zao kujitangaza mambo mazuri ambayo wamekuwa wakiyafanya.

"Jeshi la Magereza nchini kuna mambo makubwa mnayafanya katika uzalishaji lakini hamayatangazi kabisa tumieni vitengo vyenu vya habari kujitangaza ili watu wajue nini kinafanyika katika wizara yetu"alisema

Aidha, aliwataka watumishi wa wizara hiyo kuwa wabunifu katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku ili kuusaidia umma katika kero mbalimbali.

"Wizara yetu inagusa jamii katika kila eneo lazima tuwe wabunifu ili kuisadia jamii yetu kwani mtu ukifanya vizuri watu wanaona kama ambavyo yule ambaye waziri amempandisha cheo kutoka Kopro hadi Mkaguzi Msaidizi"alisema

Pia, aliagiza maofisa wote waliopandishwa vyeo mishara yao iongezeke ili kuondokana na malalamiko ambayo yamekuwepo.

"Pale ofisini ninayo malalamiko ya watu kustafu wakiwa na vyeo vikubwa lakini mishara ipo chini hivyo wanaopandishwa vyeo lazima na mishara yao isome kulingana na vyeo vyao na nitafuatilia hili," alisema.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Habari wizara hiyo, Christina Mwangosi, alisema lengo la mkutano huo ni kubadilishana uzoefu baina ya vyombo vya usalama ili kujengeana uwezo na kuongeza ufanisi katika majukumu ya kazi.



Mkuu wa Mkoa Singida, Peter Serukamba (kushoto), akizungumza na viongozi na wananchi baada ya kukagua ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Msingi Mughamo, Halmashauri ya Wilaya Singida jana, ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kukagua miradi ya maendeleo. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Kanisa launga mkono mapambano ndoa jinsia moja

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Makanisa ya Rivival Evangelistc Assemblies Of God Tanzania, Yareld Lesilwa amesema wanaunga mkono jitihada za serikali kupinga vitendo vya mmomonyoko wa maadili nchini ikiwemo ndoa za jinsia moja.

Alisema hayo juzi jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mambo mbalimbali yanayoendelea nchini.

"Hivi sasa hali ni mbaya sana sisi tunamuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan kwa asilimia mia kupinga vitendo hivi vya mmomonyoko wa maadili ambavyo ni aibu kwa taifa letu," alisema Askofu Lesilwa

Askofu huyo alisema msimamo wao ni kwamba hawaungi mkono vitendo hivyo vya ndoa za jinsia moja ambavyo ni kunyume na mpango wa Mungu.

"Sisi tutaendelea kupinga mambo haya bila ya kupepesa macho na tunaungana na serikali yetu kukemea vitendo hivi ikiwemo vile vya ukatili wa kijinsia kama ulawiti kwa watoto na ubakaji, tutaendelea kukemea mambo haya ndani ya kanisa na nje ya kanisa,"alisema

Aidha, alisema wanamunga mkono Rais katika jitihada za kupambana na dawa za kulevya, ufisadi na mambo mengine mengi ambayo hayana sura nzuri kwa Watanzania.

Pia, alimpongeza Rais Samia kwa jitihada za kulinda amani na utulivu ulipo nchini ambao unawezesha kila mtu kuabudu kwa imani yake bila ya kuvunja katika ya nchi.

"Vile vile, tunampongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kukamilisha miradi iliyoachwa na mtangulizi wake Hayati Rais John Magufuli ikiwemo ujenzi wa Ikulu, Bwawa la Mwalimu Nyerere pamoja na ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), barabara na miradi mingine mingi," alisema.

Kwa mujibu wa Askof Leilwa kanisa hilo lilianzishwa baada ya mgogoro uliodumu kwa takribani miaka sita katika Kanisa la EAGT, hali iliyosababisha baadhi yao kuondoka na kuanzisha huduma mpya.

Hata hivyo alisema wanaishukuru serikali kwa kuwapatia usajili ya muda ambao umewawezesha kuanzisha kanisa hilo ambalo hivi sasa limeenea nchi nzima.





# Serikali kujenga mabwawa sita kupunguza migogoro

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

SERIKALI inatarajia kujenga mabwawa sita ya kuvuna maji kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kibinadamu ikiwamo kilimo, ufugaji na matumizi ya nyumbani katika Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya ili kupunguza migogoro ambayo imekuwa ikisababishwa na ukosefu wa maji.

Wilaya ya Mbarali ni miongoni mwa wilaya zinazoongoza kwa uzalishaji wa mpunga nchini lakini imekuwa ikikabiliwa na migogoro mbalimbali ya matumizi ya maji ikiwamo migogoro ya wakulima na wafugaji, wakulima kwa wakulima na wakulima wadogo na wawekezaji.

Aidha wilaya hiyo imekuwa ikikabiliwa na migogoro kati ya wafugaji na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kutokana na baadhi ya wafugaji kuingiza mifugo hifadhini kwenda kutafuta malisho na maji kwa ajili ya mifugo yao.

Mbunge wa Mbarali, Francis Mtega aliyasema hayo kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kata ya Chimala wilayani humo ambapo alisema serikali imeahidi kujenga mabwawa hayo katika maeneo mbalimbali.

Alisema mabwawa hayo yatakuwa yanatumika kuvuna maji ya mvua kipindi cha masika na kutumika kwenye shughuli mbalimbali kipindi cha kiangazi ambacho ndicho huwa na tatizo kubwa la maji katika maeneo mengi.

Mtega alisema wakati wa ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan mwaka jana wilayani humo aliomba wananchi kujengewa mabwawa ili kuondoa migogoro ya mara kwa mara na ombi hilo limesharidhiwa na serikali.

"Mnakumbuka siku Rais Samia ametoka kwenye Maonyesho ya Nanenane, nilimuomba tujengewe mabwawa ya maji kwa ajili ya umwagiliaji na nilifafanua kuwa licha ya kuwa tutamwagilia mashamba yetu ya mpunga lakini maji hayatutoshi akaahidi kutusaidia na sasa tayari ameridhia tunasubiri wataalamu waanze kazi," alisema Mtega.

Alisema mabwawa yatakayojengwa mbali na kuwasaidia wananchi wa wilaya hiyo pia yatasaidia kupunguza migogoro kwenye Mto Ruaha Mkuu unaopeleka maji kwenye mabwawa ya Mtera na bwawa la Mwalimu Julius Nyerere.

Vilevile alisema mabwawa hayo yatachochea shughuli za uvuvi wa samaki katika wilaya hiyo na kuboresha lishe kwa wananchi pamoja na kuchochea biashara.

Katika hatua nyingine Mtega alisema msimu wa kilimo uliopita zaidi ya ekari 400 za mashamba ya mpunga wilayani humo zilikuwa hatarini kuharibika kwa kukosa maji kutokana na kukosa maji hali iliyomlazimu kuacha vikao vya Bunge na kwenda mara kwa mara kutafuta ufumbuzi.

Alisema juhudi nyingine zilizofanywa na serikali ni kuboresha skimu za umwagiliaji zilizokuwa zimechakaa na kusababisha upotevu mkubwa wa maji ikiwamo skimu za Igumbilo na Isenyela.

Baadhi ya wananchi wa wilaya hiyo waliishukuru serikali kwa uamuzi huo wakieleza kuwa hali imekuwa mbaya katika miaka ya sasa kutokana na mahitaji ya maji kuongezeka katika wilaya hiyo.

Mmoja wa wananchi hao, Salion Ole Kurupashi ambaye ni mfugaji katika eneo la Itamboleo alisema kipindi cha kiangazi huwa wanahangaika kutafuta maji ya kunywesha mifugo yao hali ambayo inawaingiza kenye migogoro na wakulima.

Alisema mabwawa yanayojengwa na serikali yatasaidia kuondoa migogoro yote inayowasumbua hasa inayohusiana moja kwa moja na maji.

"Sisi wafugaji tunahitaji maji kwa ajili ya mifugo yetu na wenzetu wakulima wanayahitaji kwa ajili ya umwagiliaji, lakini pia serikali nayo ina mipango yake, kwa hiyo tunajikuta tunakuwa na migongano ya mara kwa mara," alisema Ole Kurupashi.

Naye Yona ambaye ni mkulima wa mpunga katika Bonde la Usangu alisema mabwawa hayo yatasaidia kuongeza uzalishaji wa mpunga katika maeneo yao kwa maelezo kuwa maeneo ya uzalishaji yataongezeka.

Alisema wakulima wengi huwa wanalima mara moja kwa mwaka kutokana na kukosekana kwa huduma ya maji ya kutosha hali ambayo sasa inakwenda kutatuliwa.

# Neema kwa madereva Uber, Tigo zikishirikiana

**Na Mwandishi Wetu**

MADEREVA bajaji, taxi na bodaboda kuanza kupata neema baada ya kampuni ya usafirishaji mtandaoni ya Uber kuingia makubaliano na kampuni ya huduma za simu ya Tigo, kwamba wataweza kupokea malipo ya nauli kwa mfumo wa lipa kwa simu.

Uber yenye mtandao wa madereva zaidi ya 5,000 nchini imeamua kumpunguzia abiria ulazima wa kulipa kwa pesa taslimu na kutoa fursa kwa madereva ya kujiongezea kipato kupitia mfumo huo.

Akizungumza jana kwa niaba ya Meneja wa Uber Afrika Mashariki, Imran Manji, Meneja Uwendeshaji wa Uber hapa nchini, Monica Mziray alisema madereva wa Uber watakaokuwa wamesajiliwa kwenye mfumo wa mawakala wa lipa kwa simu watapata asilimia 20 ya ada ya malipo kwa kila muhamala utakaofanywa na abiria.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Huduma ya Tigopesa kutoka kampuni ya Tigo, Angelica Pesha, alisema kwa abiria atakayetumia huduma hiyo atarudishiwa kwenye akaunti yake ya tigopesa asilimia 10 ya nauli atakayolipa kwa kila safari.

Alisema mpaka sasa kuna mawakala 250,000 wanaotumia huduma ya lipa kwa simu na kuna miamala ya Sh. bilioni tatu inafanyika kila siku kupitia huduma hiyo.



Mkuu wa Wilaya ya Korogwe mkoani Tanga, Jokate Mwegelo, akimwaga zege wakati wa ujenzi wa nyumba ya walimu katika Shule ya Msingi Magila Gereza, alipofanya ziara ya kukagua miradi mbalimbali wilayani humo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi waomba elimu ya ardhi kuepuka migogoro

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WANANCHI wilayani Mbarali mkoani Mbeya wameiomba serikali pamoja na wasaidizi wa kisheria kuitisha mikutano ya mara kwa mara kuanzia ngazi ya vitongoji kwa lengo la kutoa elimu kuhusu matumizi ya ardhi.

Wamesema hali hiyo itasaidia kukabiliana na migogoro ya ardhi inayoikumba wilaya hiyo.

Walitoa ombi hilo kwenye mkutano ulioandaliwa na Kituo cha Wasaidizi wa Msaada wa Kisheria (RSCO) kwa kushirikiana na serikali ya wilaya, ulio lenga kuwaelimisha wananchi kuhusu sheria na taratibu za matumizi sahihi ya ardhi.

Mmoja wa wananchi hao, Elizabeth Michael alisema uelewa duni wa masuala ya kisheria umechangia kwa kiasi kikubwa uwepo wa migogoro ya ardhi baina ya wananchi kwa wananchi na serikali na wananchi kutokana na wananchi wengi kuvunja sheria kwa kuingia kwenye maeneo yaliyotengwa, kuendesha shughuli za kilimo na ufugaji.

Osward Linus alisema pamoja na kumiliki ardhi lakini hana uelewa wa kutosha juu ya sheria za ardhi na kwamba baadhi ya wananchi wanaokwenda ngazi za juu kuhitaji msaada wa utatuzi wa migogoro hushindwa kupata haki zao kutokana na kushindwa kujieleza vizuri, hivyo uwepo wa mikutano hiyo utawajengea ujasiri wananchi.

Fetina Fungo alisema tatizo kubwa wanalokutana nalo ni migogoro ya ardhi kati ya wafugaji na wakulima kutokana na kuwa makundi hayo huendesha shughuli hizo pasipo kuzingatia sheria na taratibu za matumizi sahihi ya ardhi.

Ofisa Ardhi wa Wilaya ya Mbarali, Geofrey Mwaijobele, alisema kutokana na ongezeko la watu, wananchi wa eneo hilo wametambua umuhimu wa umiliki wa ardhi kisheria.

Alisema migogoro mingi ya ardhi imekuwa ikisababishwa na uelewa mdogo wa kisheria kwa wananchi waliowengi.

Aliwashukuru maofisa wa RSCO kwa kufanya mkutano huo na kuwaomba kuendelea kufanya mikutano mingine kuanzia ngazi ya vitongoji, vijiji na kata kwa madai kuwa serikali peke yake haiwezi kutoa elimu na kutatua migogoro hiyo.

Mkurugenzi wa RSCO, Edson Mwakyembe, alisema wanalenga kuisaidia serikali kutatua migogoro ambayo inaweza kumalizwa ngazi za chini za maamuzi.

# DK. Mwinyi ahimiza watunza kumbukumbu kuwezeshwa

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali inawajibu wa kutenga bajeti ya kuwawezesha watumishi wa umma hususani kada ya watunza kumbukumbu.

Aliyasema hayo jana Ikulu, Zanzibar alipozungumza na uongozi wa Chama Cha Menejimenti ya Kumbukumbu na Nyaraka Tanzania (TRAMPA).

Alisema bado serikali ina wajibu wa kuwapeleka masomoni na kuwaongezea uwezo watunza kumbukumbu na watumishi wengine wa umma ili kuwajengea uweledi katika kukidhi haja ya taaluma zao.

Alisema TRAMPA ni mfano wa kuigwa na taasisi nyingine nchini ambacho kimejikita kwenye weledi wa hali ya juu wa kuwainua wanachama wake kitaaluma na ufanisi.

Dk. Mwinyi, alitumia fursa hiyo kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa uamuzi wa kuuleta mkutano wa TRAMPA kwenye visiwa vya Zanzibar na kusema kuwa mbali na kufanikisha malengo ya mkutano huo pia umeakisi dhima ya utalii wa ndani.

Dk. Mwinyi alisema asilimia 30 ya uchumi wa Zanzibar unatokana na sekta ya utalii, hivyo mkutano wa TRAMPA uliinufaisha Zanzibar kiuchumi na biashara hasa kwa sekta za umma, binafsi na wananchi wa kawaida.

Dk. Mwinyi alisema, Zanzibar na Tanzania Bara kuna ushirikiano mkubwa katika kuitangaza na kuishajihisha sekta ya utalii hususani wageni na watalii wanaoitembelea Tanzania.

Alisema: "Hapa Zanzibar tuna jambo moja ambalo tunalitumia vizuri, kwamba wageni wanaotaka kwenda kwenye mbuga, kule Tanzania Bara kwa uwindaji au iwe safari tu za kuangalia wanyama, aidha wanaanza kule lakini kisha lazima waje Zanzibar na wakianza huku lazima waende Tanzania Bara".

Aidha alisema, Tanzania imeweka utaratibu mzuri wa kuendelea kuutangaza utalii na kueleza kuwa kitu ambacho kimeunganisha na kuendelea kuweka nguvu zaidi ili watalii wote wanaokuja Tanzania japo kwa siku chache wapate nafasi ya kufika Zanzibar na wanaoanzia Zanzibar wafike Tanzania Bara.

Dk. Mwinyi alisema faida za mkutano wa TRAMPA visiwani Zanzibar uliwanufaisha wazawa wengi kuanzia wafanyabiashara wenye maduka, vyakula, hoteli, nyumba za wageni hata sekta ya usafirishaji wakiwamo madereva taxi, bodaboda, daladala na wafanyabiashara wengine.

Mwenyekiti wa TRAMPA, Devota Mrope aliiomba Serikali ya Zanzibar kutoa ushirikiano kwa kuwaruhusu watunza kumbukumbu wake kuhudhuria mafunzo yatakayoandaliwa na chama hicho ndani na nje ya Zanzibar ili kuwaongezea weledi na uwezo wa kitaaluma watumishi hao.

# Wizara ya Utalii yaanika vipaumbele 4 kuvutia watalii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar imetaja vipaumbele vinne itakavyovitekeleza kwa mwaka fedha 2023/2024 ambavyo vitakavyosaidia kuongeza idadi ya watalii na pato la taifa.

Akiwasilisha bajeti ya wizara hiyo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Waziri wa wizara hiyo, Simai Mohammed Said alisema mojawapo ya vipaumbele hivyo ni kuendelea kuitangaza Zanzibar kimataifa kwa lengo la kutafuta masoko mapya yatakayochangia kukuza utalii wa nchi.

Alisema vingine ni kuandaa mfumo wa kidijitali katika kuboresha huduma za sekta ya utalii na mambo ya kale, kuendelea kusimamia utekelezaji wa mradi wa ukarabati wa jengo la Beit el Ajaib ili liweze kurudi katika hali yake ya awali.

**Siku za ukaazi kwa wageni zimeongezeka kutoka siku saba kwa mwaka 2019 hadi kufikia siku nane kwa Machi, 2023.**

"Tunaendelea na utekelezaji wa mradi wa kuimarisha maeneo ya kihistoria yakiwamo, eneo la kihistoria la Ras Mkumbuu, Mangapwani, Maruhubi, Mahamamu ya Kidichi, Hamamni, Forodhani na Kizimbani pamoja na kuweka maonyesho katika majengo yaliyokamilika ujenzi wake kama vile Bungi kwa Bikhole, Mwinyi Mkuu Dunga, Fukuchani, Mvuleni, Mkamandume, Chwaka Tumbe, Pango la Kijiji na Makumbusho ya Amani na Makumbusho ya viumbe hai," alisema.

Waziri Simai alisema watalii walioingia nchini mwaka 2022 ni asilimia 39 kutoka watalii 394,185 mwaka 2021 hadi kufikia watalii 548,503 mwaka 2022.

Alisema ongezeko hilo linatokana na juhudi zinazochukuliwa na serikali katika kuitangaza nchi kitaifa na kimataifa.

Aidha, alisema siku za ukaazi kwa wageni zimeongezeka kutoka siku saba kwa mwaka 2019 hadi kufikia siku nane kwa Machi, 2023.

Hata hivyo alisema wizara imepokea meli tano kubwa za kitalii ambazo ni Zaandam, MS Coral, Geographer, Le Jacques Cartier na MV Seaborne ambapo ziliwasili nchini na kushusha watalii 2,000 ambao wamepata fursa ya kuvitembelea vivutio vya kitalii ikiwamo mashamba ya viungo, Msitu wa Jozani na maeneo ya Mji Mkongwe.

Waziri huyo alisema wizara kupitia Kamisheni ya Utalii kwa upande wa Pemba imefanikiwa kuongeza idadi ya watalii walioingia kisiwani humo kutoka watalii 14,548 mwaka 2021 hadi kufikia watalii 27,826 kwa mwaka 2022 sawa na ongezeko la asilimia 91.



Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Simai Mohammed Said akizungumza wakati akiwasilisha bajeti ya wizara yake kwa mwaka wa fedha 2023/2024, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kina cha maji chakwamisha meli

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi imesema kutoanza kwa safari za meli kwa Bandari ya Mkokotoni Mkoa wa Kaskazini Unguja kumetokana na uwapo wa tatizo la kina kidogo cha maji.

Imesema tatizo hilo linasababishwa na mwelekeo wa maji unaosababisha kujaza mchanga sehemu iliyochimbwa, kupata kina kirefu cha maji.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Nadil Abdullatif, alitoa ufafanuzi huo juzi wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi akijibu swali la mwakilishi wa Kiwani, Mussa Foum.

Foum alitaka kujua ni sababu zipi zinazosababisha kutoanza kwa safari za meli katika bandari hiyo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Abdullatif alisema wizara yake inaendelea kutafuta njia mbadala ili kutatua tatizo hilo, ikiwezekana kufanya mabadiliko ya mwelekeo wa maji.

Alisema: "Mheshimiwa Spika, huduma katika Bandari ya Mkokotoni itapatikana baada ya kufanyia kazi matatizo yaliyojitokeza pamoja na kumalizia ujenzi kwa sehemu zilizobakia."

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## TANGAZO LA KAZI IT ANAHITAJIKA

IT ngazi ya certificate au diploma msichana kati ya miaka 20 Hadi 25 kituo Cha kazi chamazi Temeke

**TUPIGIE: 0753 38 28 33**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**GOODCHANCE ANDARSON KISANGA** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T313 CNZ .** Chasses Namba **DD51T589561** , Engine Namba **F6A6813788** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . Polisi Taafifa : **KIL/MOS/RB/154627/2023**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**JAQUELINE G. TARIMO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.357/41** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **URU SEKONDARI** mwaka **1989.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/KIM/RB/184323/2023.**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**SABINA GEORGE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.324/9 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **LINDI SEKONDARI** mwaka 1985. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/STA/RB/122966/2022.**

**FORM NO. 58**
**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO. 57 OF 2023**

**In Matter of the Estate of the Late**
**RAPHAEL KALEBI KAAYA**

**By 1. EKANDE RAPHAEL KAAYA**
**2. ................................**

All Persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or latter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the **13 / 06 / 2023.**
Dated at **Morogoro**, this **30** day of **05, 2023**

RESIDENT MAGISTRATE

**FORM NO. 58**
**IN THE COURT OF DISTRICT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO. 3 OF 2023**

**In Matter of the Estate of the Late**
**MATHEW LEONARD MHUTO**

**In Matter of Application for letters of administration by**
**FLORA METHEW MHUTO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

All Persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the **03 / 07 / 2023**
Dated at Dar es Salaam, this **16** day of **05, 2023**

Senior Resident Magistrate

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0677020701**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 0677020701**

**E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**

**WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Jeshi Sudan lasitisha mazungumzo na RSF

**KHARTOUM, Sudan**

JESHI la serikali ya Sudan limesitisha ushiriki wake katika mazungumzo ya kusimamisha mapigano kati yake na wanamgambo wa Kikosi cha Msaada wa Haraka (RSF) yanayosimamiwa na Marekani na Saudi Arabia.

Akizungumza kwa sharti la kutotambulishwa, ofisa wa serikali aliyezungumza na AFP, alisema Jeshi la Serikali lilichukuwa uamuzi huo kwa sababu kundi la RSF halijawahi kutekeleza hata sharti moja la mkataba wa muda mfupi wa kusitisha mapigano.

Mkataba huo ulitaka kuondoka kwa kikosi cha RSF katika hospitali na majengo ya makazi.

Aidha, wapatanishi wa Marekani na Saudi Arabia walisema kuwa jeshi la serikali na kikosi cha RSF walikuwa wamekubaliana kuongeza muda wa siku tano katika mkataba wa msaada wa kibinadamu ambao ulikiukwa mara kwa mara katika wiki iliyotangulia.

Ilielezwa kuwa licha ya ahadi zao, mapigano yalizuka tena Jumanne jioni katika maeneo ya Khartoum na Magharibi mwa Darfur.

Kiongozi wa Jeshi la serikali Abdel al- Burhan, wakati alipowatembelea wanajeshi wake katika mji mkuu wa Khartoum, alisema kuwa jeshi hilo liko tayari kupigana hadi kupata ushindi.

Kiongozi wa RSF Mohamed Daglo, ambaye kwa sasa ni hasimu mkubwa wa Burhan, alisema kwamba kikosi chake kitatekeleza haki yake ya kujilinda na kulishtumu Jeshi la serikali kwa kukiuka mkataba.

***DW***

**Kiongozi wa Jeshi la serikali Abdel al-Burhan, wakati alipowatembelea wanajeshi wake katika mji mkuu wa Khartoum, alisema kuwa jeshi hilo liko tayari kupigana hadi kupata ushindi.**

# Uganda yazijibu nchi za Magharibi

**KAMPALA, Uganda**

UGANDA imelaani majibu ya mataifa ya Magharibi ikiwemo Marekani kwa sheria mpya dhidi ya ushoga inayochukuliwa kuwa moja ya sheria kali duniani, ikisema kwamba vitisho vya vikwazo kutoka kwa wafadhili ni udanganyifu.

Sheria iliyosainiwa juzi na Rais Yoweri Museveni inatoa adhabu ya kifo au kifungo cha maisha kwa mtu atakayejihusisha na mapenzi ya jinsia moja, sheria ambayo imekemewa na serikali za Magharibi na kuhatarisha baadhi ya mabilioni ya dola za misaada ya nje ambayo nchi hiyo inapokea kila mwaka.

Rais wa Marekani Joe Biden alitishia kupunguza misaada na kuiwekea nchi hiyo vikwazo vingine, huku Waziri wa Mambo ya Nje Antony Blinken akisema serikali itazingatia viza dhidi ya maofisa wa Uganda.

Aidha, baada ya kauli hizo za Marekami, Mbunge wa Bugiri nchini Uganda, Asuman Basalirwa aliwataka wabunge na Waganda kwa ujumla, kutoyumbishwa na hatua zinazochukuliwa na nchi za magharibi baada ya Bunge la nchi hiyo kupitisha sheria mpya dhidi ya ushoga.

Basalirwa, alitoa wito huo baada ya ubalozi wa Marekani nchini humo kubainisha kuwa taifa hilo kubwa duniani limeifuta pasi ya kusafiria (VISA) ya Spika wa Bunge la Uganda Anita Among, huku akisisitiza kuwa maamuzi yaliyofanyika juu ya kupitishwa kwa sheria hiyo ni azimio la Waganda.

"Tumepata taarifa kuwa ubalozi wa Marekani nchini Uganda, umemfutia Spika wa Bunge Anita Among viza yake lakini hili ni azimio la Waganda, tunapaswa kushikilia msimamo kwani ni hatua kuu iliyofikiwa na hatupaswi kudhoofishwa," alisema na kuongeza;

"Nadhani walitafuta kujua kama nina viza ya Marekani na hawakupata, kwa hiyo, mwathirika wa kwanza ni spika, ninaelewa serikali ya Uingereza nayo iko mbioni kufanya hivyo, kwanza hatuna tatizo na namna nchi hiyo inavyosimamia mambo yake," alisema Basalirwa.

"Ikiwa kwa hekima na demokrasia yao hawatutaki katika nchi zao, hiyo ni haki yao na isitokee mtu yeyote kuilaumu Marekani au Uingereza kwa kitendo chao cha kufuta viza, sitalalamika, wala kuchukia ubalozi wowote kwa kufuta visa ya mtu yeyote," alisema Basalirwa.

Naye Mkuu wa sera za mambo ya nje wa Umoja wa Ulaya (EU) Josep Borrell, alisema sheria hiyo itaathiri uhusiano wa Uganda na washirika wa kimataifa.

Hata hivyo, hayo yalitajwa kama maoni ya awali ya kina kutolewa kwa serikali ya Uganda, tangu Rais Museveni asaini sheria hiyo, na kwamba Waziri wa Habari Chris Baryomunsi alipuuza lawama hizo.

"Hatuuoni ushoga kama haki ya kikatiba, ni upotevu tu wa kijinsia ambao hatuungi mkono kama Waganda na waafrika," alisema Chris.

"Wakati tunathamini msaada tunaoupata kutoka kwa washirika, lazima wakumbushwe kwamba sisi ni nchi huru na hatutungi sheria kwa ajili ya nchi za Magharibi, tunatunga sheria kwa ajili ya watu wetu hapa Uganda, kwa hivyo usaliti wa aina hiyo haukubaliki," alisema Chris.

Vile vile, ilielezwa kuwa wanaharakati na mawakili nchini Uganda walifungua kesi mwanzoni mwa wiki hii kuipinga sheria hiyo, wakieleza kuwa inahimiza ubaguzi na unyanyapaa na kudai kuwa sheria hiyo imepitishwa bila ya kuushirikisha umma ipasavyo.

***VOA***




Wafuasi wa upinzani Uturuki wakiandamana baada ya waangalizi wa vyombo vya habari nchini humo, kutangaza kuchunguza vituo sita vya televisheni vya upinzani kwa madai ya kutukana umma kupitia matangazo ya awamu ya pili ya uchaguzi wa rais uliofanyika mwishoni mwa juma lililopita. **PICHA:AP.**

# Wakenya zaidi ya Mil 4 wakabiliwa na njaa

**NAIROBI, Kenya**

SHIRIKA la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) limesema licha ya kuwa mvua imeanza kunyesha katika baadhi ya maeneo nchini Kenya, lakini zaidi ya raia milioni nne katika taifa hilo bado wanakabiliwa na athari za baa la njaa.

Taarifa iliyotolewa na shirika hilo hivi karibuni, ilisema linaongeza hatua zake za dharura kusaidia maelfu ya Wakenya walioathiriwa na athari za takriban miaka mitatu ya ukame.

Ilieleza kuwa shirika hilo linalenga kusaidia zaidi ya watu 940,000 walioathiriwa na ukame ikiwa ni ongezeko kutoka karibu watu 600,000 kwa mwaka 2022.

Inabainishwa kuwa ukame wa muda mrefu zaidi katika historia ya pembe ya Afrika, umewaacha watu milioni 4.4 nchini Kenya wakikabiliwa na njaa, na kwamba takriban watoto na wanawake milioni 1.5 wana utapiamlo na karibu mifugo milioni tatu ilikufa.

Kupitia kwa mpango wake wa lisha jamii, WFP inalenga kuwafikia raia hao wanaokabiliwa na baa la njaa hadi pale wakulima watakapoanza kuvuna mimea yao, likieleza kuwa walionufaika na mpango huo ni raia wa Turkana, kaskazini mashariki mwa taifa hilo.

Pia ilielezwa kuwa WFP kwa kushirikiana na Shirika la Marekani la Msaada wa Kimataifa (USAID) wanalenga kuzisaidia familia zilizoathirika kwa kuwapa fedha, vyakula kama mtama, mafuta ya kupikia, mchele na uwele kwa miezi sita.

Serikali ya Kenya kwa ushirikiano na mashirika mengine ya misaada, nayo pia imeanzisha mchakato wa kuwasaidia raia wake wanaokabiliwa na njaa.

***RFI***

# Waziri, vijiji vyenye migogoro Hifadhi ya Serengeti wayajenga

**Na John Mapepele**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, amekutana na kufanya vikao na wananchi wa vijiji vyenye migogoro ya mipaka na Hifadhi ya Taifa Serengeti.

Baada ya kukutana na wananchi hao, waziri huyo ameutaka uongozi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) kuimarisha programu za ujirani mwema na kuwashirikisha wananchi wanaozunguka hifadhi wakati wa kupanga mipango yao ili wananchi washiriki kikamilifu katika uhifadhi wa rasilimali hizo na kupunguza migogoro isiyo ya lazima.

Waziri Mchengerwa alitoa maagizo hayo juzi alipozuru katika Wilaya ya Tarime na kufanya mikutano katika vijiji vyote vinavyozunguka Hifadhi ya Taifa Serengeti vilivyokuwa na migogoro na mipaka katika uwekaji wa vigingi vya mipaka.

Wananchi wa maeneo hao walipongeza hatua hiyo ya serikali kwenda kuwasikiliza na kuahidi kushirikiana nayo katika uhifadhi.

Waziri Mchengerwa alifuatana na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara yake, Anderson Mutatembwa na Kamishna wa TANAPA, William Mwakilema na kupokewa na uongozi wa Mkoa wa Mara, uongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Tarime na Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara.

Katika mikutano yote na wanakijiji, waziri Mchengerwa aliongoza vikao hivyo kwa kuwapa wasaa wananchi kutoa maoni na mawazo yao na mwisho alitolea ufafanuzi hoja hizo na nyingine kuzichukua kwa hatua zaidi.

Wananchi walipongeza hatua hiyo ya Waziri Mchengerwa kwenda kuwasikiliza huku wakieleza kuwa kumekuwa na ushirikishwaji mdogo na kuiomba serikali kupanga nao kwa pamoja ili kuondoa migogoro isiyo ya lazima.

Diwani wa Nyanungu, Tiboche Richard, alisema wananchi wa kata yake wapo tayari kushirikiana na serikali katika kila jambo endapo watashirikishwa na hifadhi.

"Mheshimiwa waziri, ninapenda kukuhakikishia kuwa leo (juzi) unatufanya tulale usingizi maana umetumwa na Mheshimiwa Rais wetu kuja kutujengea uhusiano mzuri na sisi hiki ndicho tulichokuwa tunakikosa," alisisitiza diwani huyo.

Akiwa katika Kijiji cha Karakatonga wilayani Tarime, Waziri Mchengerwa aliutaka uongozi wa TANAPA kushuka chini kwa wananchi na kwenda kuzungumza nao kwa kuwa hifadhi hizo ni za wananchi ambao ndiyo wahifadhi namba moja.

Alisema wazo la uhifadhi wa rasilimali nchini liliasisiwa miaka mingi na uongozi katika awamu zote toka enzi za Baba wa Taifa hadi Rais Samia limezingatiwa kwa faida ya kizazi cha sasa na baadaye.

Akiwa katika Kijiji cha Kegonga, Waziri Mchengerwa alitoa wito kwa wananchi hao kushirikiana na uongozi wa serikali wakati wote na kuacha tabia za kugomea kwa kuwa kwa kufanya hivyo wanachochea migogoro.

Waziri huyo aliwataka kutambua kuwa wahifadhi ni sehemu ya jamii yao kwa kuwa baadhi ya watumishi hao ni sehemu ya familia zao na watoto wao.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, akizungumza na wananchi kutoka vijiji vinavyopakana na Hifadhi ya Taifa Serengeti wilayani Tarime juzi. **PICHA: JOHN MAPEPELE**

## Taasisi mahsusi ya mikopo kwa makundi maalum yaja

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI inatarajia kuanzisha taasisi mahsusi ya fedha itakayosimamia upatikanaji na utoaji wa mikopo kwa makundi maalum.

Makundi hayo ni ya vijana, wanawake, watu wenye ulemavu na wafanyabiashara wadogo.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Chande, alibainisha hayo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Lucy Sabu.

Mbunge huyo alihoji lini serikali itaanzisha benki ya vijana wajasiriamali, Chande akijibu serikali ipo katika hatua ya kuandaa mkakati wa upatikanaji wa mitaji kwa wajasiriamali wadogo.

Alisema mkakati huo utawezesha vijana kupata mitaji kupitia benki, taasisi za huduma ndogo za fedha, masoko ya mitaji, mifuko na programu za serikali za uwezeshaji wananchi kiuchumi.

"Katika hatua ya utekelezaji wa mkakati huu, serikali inatarajiwa kuanzisha taasisi mahsusi ya fedha itakayosimamia upatikanaji na utoaji wa mikopo kwa makundi maalum wakiwamo vijana, wanawake, watu wenye ulemavu na wafanyabiashara wadogo wakiwamo machinga," alisema.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alisema katika mkutano wa vijana uliofanyika mkoani Mwanza, Rais Samia Suluhu Hassan aliahidi serikali itaanzisha benki hiyo.

"Ninaomba kujua hatua gani zimefikiwa katika uanzishaji wa benki hii?" alihoji.

Chande alijibu kuwa suala hilo lipo katika hatua ya majadiliano katika kikao kazi cha makatibu wakuu na watajulishwa hatua itakayofuata.

**Mkakati huo utawezesha vijana kupata mitaji kupitia benki, taasisi za huduma ndogo za fedha, masoko ya mitaji, mifuko na programu za serikali za uwezeshaji wananchi kiuchumi.**

# Makamba: Kila kijiji kupata umeme mwakani

**Na Elizabeth Zaya,** DODOMA

WAZIRI wa Nishati, January Makamba amesema ifikapo mwezi Juni mwakani, vijiji vyote Tanzania vitakuwa na umeme.

January alitangaza hayo jana katika maonyesho ya Wiki ya Nishati yanayofanyika katika Viwanja wa Bunge jijini hapa.

Alisema mipango hiyo ya kufikia vijiji vyote inatokana na mikakati iliyowekwa na serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi katika kuwekeza kwenye sekta hiyo kusaidia kufikia malengo kwa wakati.

"Tunachokifanya sasa hivi ni kuongeza vyanzo vingine na kupunguza utegemezi wa maji, ili kwanza kuondokana na shida zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi, pia kuwa na gridi ambayo ni imara zaidi.

"Sisi tumebarikiwa kuwa na rasilimali za asili nyingi za kuzalisha umeme na tutazitumia zote, nia ni kwamba ikitokea chanzo kimoja kimepata shida, kingine kinaendelea kufanya kazi.

"Watu wanalalamika kukatika umeme. Rais Samia Suluhu Hassan ameidhinisha Sh. trilion 1.9 ya kufanya miradi 26 na miradi ambayo imeanza. Kwa hiyo, niwahakikishie wananchi umeme wa uhakika," alisema.

Waziri huyo alisema dhamira ya wizara hiyo ni kushamirisha na kuziwezesha sekta nyingine zote za uzalishaji kutimiza malengo yake.



Pia wanatarajia kuingiza umeme wa jua na tayari wametia saini mkataba kwa ajili ya kuanza kazi hiyo.

"Tumeshatia saini mkataba wa kuingiza umeme wa jua katika gridi kwa mara ya kwanza. Sasa hivi ukitazama mchanganyiko wa vyanzo katika gridi yetu, utaona sasa maji yako chini, gesi ndio inaongoza asilimia 65 na maji asilimia 30. Tayari tunaweka mikakati ya kupunguza utegemezi wa maji.

"Kwa mara ya kwanza tutaingiza umeme wa jua wa Megawati 50 katika gridi ya taifa, juzi tumetia saini mkataba kwa ajili hiyo, mradi huu uko Kishapu mkoani Shinyanga.

"Ndani ya miezi 12 mpaka 18 umeme wa jua na wa upepo utekelezaji wake utaanza kwa sababu tunataka kuufanya kwa haraka," alisema.

Pia alisema katika kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa umeme, nguvu kubwa inatarajiwa kuwekezwa katika vyanzo vingine vya joto ardhi.

## ZISIKUPITE

### BENZEMA KUHAMA
MSHAMBULIAJI wa Real Madrid Karim Benzema anafikiria kuihama timu hiyo baada ya kupata ofa ya mkataba wa miaka miwili yenye thamani ya euro milioni 400 kutoka Saudi Arabia kwa ajili ya kumnunua Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 35. ***(ESPN)***

### ROWE HAUZWI
ARSENAL haina nia ya kumuuza Emile Smith Rowe mwenye umri wa miaka 22, msimu huu wa joto na ina matumaini kuwa mshambuliaji huyo wa England ambaye amekuwa akikumbwa na majeraha ya mara kwa mara atarejea atapona na kuwa tayari kwa mashindano ya Ulaya ya vijana chini ya miaka 21, ***(Athletic)***

### ENRIQUE AWANIWA NAPOLI
KOCHA anayesakwa na Tottenham Hotspur, Luis Enrique yuko kwenye mazungumzo na mabingwa wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Napoli. Hata hivyo, kocha huyo wa zamani wa Hispania na Barcelona ana nia ya kujiunga na timu ya ligi kuu England. ***(Guardian)***

### MADDISON ASAKWA
TOTTENHAM Hotspur na Newcastle United zinapigana vikumbo kupata saini ya kiungo wa Leicester City, James Maddison mwenye umri wa miaka 26 na winga Harvey Barnes mwenye miaka 25, huku wachezaji hao wa kimataifa wa England wakiwa na thamani ya takriban pauni milioni 40. ***(Sun)***

### CAICEDO KUONDOKA
MAKUBALIANO kati ya kocha wa Brighton, Roberto de Zerbi na Moises Caicedo yatamfanya kiungo huyo wa kati wa Ecuador mwenye umri wa miaka 21 kuondoka pale Seagulls msimu huu wa joto. ***(Fabrizio Romano)***

### GNANTO AFUATILIWA
KLABU ya Manchester City na Arsenal zinamfuatilia mshambuliaji wa Leeds United na Italia, Wilfried Gnonto mwenye umri wa miaka 19. ***(Calciomercato)***

### WEGHORST HASAJILIWi
MANCHESTER United haitamsajili mshambuliaji wa Uholanzi, Wout Weghorst mwenye umri wa miaka 30, wala kiungo wa kati wa Austria, Marcel Sabitzer mwenye miaka 29 kwa mikataba ya kudumu, walikuwa United msimu uliomalizika wakitoea kwneye klabu zao za Burnley na Bayern Munich. ***(Mail)***

### FRESNEDA OFA NONO
MLINZI wa kulia wa Real Valladolid, Ivan Fresneda mwenye umri wa miaka 18, amepokea ofa nono kutoka kwa Arsenal. ***(Bild)***

### PAVARD KUONDOKA
BEKI wa Ufaransa, Benjamin Pavard mwenye umri wa miaka 27 anatarajiwa kuondoka Bayern Munich baada ya Inter Milan kuonesha nia tena ya kumtaka. ***(Fabrizio Romano)***

### ASENSIO ATAKIWA VILLA
KLABU ya Aston Villa inamtaka Marco Asensio wa Real Madrid, ambaye anatarajiwa kuondoka bure msimu huu wa joto. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania mwenye umri wa miaka 27 pia anazivutia klabu za Paris St-Germain, Arsenal na AC Milan. ***(Sun)***

### KONE AWANIWA
LIVERPOOL inataka kumnunua kiungo wa kati wa Borussia Monchengladbach, Manu Kone, mwenye umri wa miaka 22 mwenye thamani ya karibu euro milioni 40. ***(Bild)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MARTIAL KUIKOSA FAINALI YA FA

Mshambuliaji huyo asema anaamini atafikia malengo akiwa hapo na…

**MANCHESTER, England**

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Anthony Martial ameondolewa kwenye fainali ya Kombe la FA itakayochezwa Jumamosi hii dhidi ya Manchester City kutokana na jeraha la misuli ya paja.

Martial alipata tatizo hilo katika mchezo wa mwisho wa United wa Ligi Kuu msimu huu Jumapili dhidi ya Fulham na uchunguzi umeonyesha ameumia misuli ya paja.

United walisema katika taarifa yao: "Anthony Martial hatashiriki fainali ya Kombe la FA Jumamosi dhidi ya Manchester City kutokana na jeraha.

"Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa aliumia misuli ya paja kuelekea mwisho wa ushindi wa 2-1 dhidi ya Fulham Jumapili kwenye uwanja wa Old Trafford.

"Tathmini imefichua kupasuka kwa misuli ambayo inamzuia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 kutoshiriki pambano la Wembley." Martial alikosa mechi mbili za kwanza za Ligi Kuu ya England msimu huu kutokana na tatizo la misuli ya paja, huku majeraha mengine madogo madogo tangu hapo yamemzuia kucheza mechi 29 katika michuano yote ambapo amefunga mabao tisa.

Mechi 11 pekee kati ya 21 za ligi msimu huu ndizo amekuwa kwenye kikosi cha kwanza, lakini alikuwa na matumaini ya kuwa kwenye kinyang'anyiro cha kuanza Wembley dhidi ya City, ambao wanataka kukamilisha mataji matatu msimu huu.

Winga huyo wa zamani wa Lyon, ambaye alitumia kipindi cha pili cha msimu uliopita kwa mkopo akicheza kule Sevilla, alijiunga na United kutoka Monaco kwa pauni milioni 36 mwaka 2015 na ameichezea klabu hiyo takriban mechi 200 za ligi.



# POCHETTINO HAMTAKI FELIX CHELSEA

**MADRID, Hispania**

KOCHA mpya wa Chelsea, Mauricio Pochettino hataki Joao Felix abaki katika klabu hiyo msimu ujao, kwa mujibu wa Rais wa Atletico Madrid, Enrique Cerezo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 alijiunga na Chelsea Januari kwa mkopo wa miezi sita kutoka Atletico, muda mfupi baada ya kuongeza mkataba wake na klabu hiyo ya LaLiga hadi mwaka 2027.

Felix amekuwa akifanya vyema katika kipindi chake akiwa Stamford Bridge akiwa na mabao manne ya Ligi Kuu ya England katika mechi 16, lakini Cerezo alisema hataendelea kuichezea Chelsea.

Alipoulizwa kuhusu hatima ya mchezaji huyo, Cerezo aliwaambia waaandishi wa habari: "Ukweli ni kwamba siwezi kuwaambia mpango huo na Joao.

"Habari tulizozipata jana ni kwamba kocha mpya hamtegemei Chelsea. Hatuna lolote tulilopanga, Joao ni mchezaji wa Atletico kwa sasa."

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno hapo awali alidokeza kwamba mustakabali wake unategemea klabu hiyo kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, lakini Chelsea ilimaliza katika nafasi ya 12 na kukosa kucheza soka la Ulaya.

Pochettino atakuwa na jukumu la kuirejesha Chelsea barani Ulaya baada ya kusaini mkataba wa miaka miwili ya kuinoa klabu hiyo Jumatatu.

## Wanamichezo watakiwa kunywa chai kuimarisha miili

**Na Christina Mwakangale**

WANAMICHEZO nchini wameshauriwa kujenga utaratibu wa kunywa chai kwa sababu kinywaji hicho huongeza kiwango cha nishati mwilini na kuboresha ufanisi wawapo viwanjani.

Ushauri huo umetolewa jijini Dar es Salaam jana na Mshauri wa Utamaduni wa Ubalozi wa China na Mkurugenzi wa Kituo cha Utamaduni cha Watu wa China hapa nchini Wang Siping, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya unywaji chai.

Alisema unywaji wa chai baada ya kazi huinua kiwango cha metabolizimu, kupunguza maumivu ya misuli, huchoma mafuta mwilini ambayo hayahitajiki katika mwili hasa kwa wanamichezo.

"Kwa vyovyote vile katika uchezaji wako muhimu ni kujihisi mwenye nguvu lakini pia mwili kupumzika baada ya michezo, kitu kilicho muhimu ni chai ambayo inainua kiwango cha nishati ya mwili, nawashauri wanamichezo wote kuweka utaratibu wa kutumia chai," alisema Wang na kuongeza,

"Nikiwa mtu mwenye asili ya China, chai si tu ni imani kwa Wachina, lakini ni asili ya binadamu, muhimu ni kuunganisha kiungo hicho na utaratibu wako wa kila siku," alisema.

Alisema kwa taifa la China usherehekea siku ya unywaji chai ifikapo Mei 21 kila mwaka na hiyo imekuwa tiba nzuri kwa wanamichezo ambao wanaimarisha miili yao.

# Juventus yaongoza mbio kumsajili Pulisic

**TURIN, Italia**

JUVENTUS inaongoza katika mbio za kumsajili Christian Pulisic, vyanzo vimeiambia ESPN, huku Chelsea ikiwa tayari kumtoa mshambuliaji huyo wa Marekani kwa ada ya pauni milioni 20 msimu huu wa joto.

Ingawa Chelsea sasa wamethibitisha kumteua Mauricio Pochettino kama kocha mkuu mpya Stamford Bridge kwa mkataba wa miaka miwili, vyanzo vimesema ujio wa kocha huyo wa zamani wa Tottenham Hotspur na Paris Saint-Germain hautaashiria kubadilishwa kwa uamuzi wa klabu kusikiliza ofa za Pulisic.

Pulisic, aliyesajiliwa kwa pauni milioni 58 kutoka Borussia Dortmund mwaka 2019, amebakiza miezi 12 katika mkataba wake na Chelsea, huku klabu hiyo ikihitaji kupunguza ukubwa wa kikosi chao na bili ya mshahara baada ya kutumia pauni milioni 585 kununua wachezaji wapya mwaka mmoja uliopita.

Klabu nyingine zimefuatilia kuhusu uwezekano wa kumsajili Pulisic, huku vyanzo vya habari vikiiambia ESPN kwamba Manchester United, Newcastle, Napoli, AC Milan na Galatasaray zote zimefahamishwa kuhusu uwezekano wa ada na mshahara wa mchezaji huyo, ambaye analipwa pauni milioni 13 kwa mwaka.

Lakini klabu ya Juventus ya Italia imeibuka kuwa mstari wa mbele, licha ya kusita kufikia mkataba wa malipo wa Pulisic pale Stamford Bridge.



Juve, ambao hawatashiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao kufuatia kukatwa pointi 10 kwa uhasibu wa uwongo na kuwafanya wabaki nafasi ya saba kwenye Serie A, wanajaribu kuimarisha safu yao ya ushambuliaji huku mawinga Angel di Maria na Juan Cuadrado wote wakiwa wamemaliza mkataba msimu huu.

Akiwa na uzoefu wa hali ya juu katika Chelsea na Dortmund katika umri mdogo, fowadi huyo anachukuliwa kuwa chaguo la bei nafuu la pauni milioni 20 ikiwa makubaliano yanaweza kupatikana ya kupunguza mshahara wake.

Pulisic, mwenye umri wa miaka 24, amekumbana na majeraha akiwa Chelsea katika misimu miwili iliyopita.

Alizomea na baadhi ya mashabiki wa klabu hiyo alipotambulishwa kama mchezaji wa akiba wa kipindi cha pili wakati wa mchezo wa mwisho wa msimu nyumbani dhidi ya Newcastle United Jumapili.

===

HABARI MICHEZO

# AISHI MANULA AFANYIWA UPASUAJI AFRIKA KUSINI

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA wa Simba na Timu ya Taifa 'Taifa Stars', Aishi Manula, amefanyiwa upasuaji Afrika Kusini alipoenda kwa ajili ya matibabu ya majeraha ya nyama za paja.

Manula aliondoka nchini Jumatatu akiongozana na daktari wa klabu yake Edwin Kagabo kwa ajili ya kwenda kupata matibabu kutokana na jeraha lililomweka nje kwa muda mrefu.

Manula aliumia kwenye mchezo wa robo fainali ya Kombe la FA walipocheza dhidi ya Ihefu kwenye Uwanja wa Azam Complex Aprili 7 mwaka huu, na tangu hapo alikuwa nje ya uwanja huku golikipa namba tatu wa klabu hiyo, Iddi Salim akicheza kwenye michezo iliyofuata.

Meneja wa machezaji huyo, Jemedari Said amesema, golikipa huyo alifanyiwa upasuaji juzi saa saba mchana kwa saa za Afrika Kusini ambayo ni sawa na saa nane mchana kwa saa za hapa nyumbani na kwa sasa anaendelea vizuri.

"Nimewasiliana naye muda mfupi baada ya kutoka chumba cha upasuaji yupo vizuri, kilichobaki sasa ni kupangiwa ratiba ya mazoezi pale daktari wake atakapoona inafaa," alisema Jemedari.

Aidha, alisema kwa sasa hajui mchezaji huyo atakuwa nje ya uwanja kwa muda gani na wanasubiri maelekezo ya madaktari waliomfanyia upasuaji.

"Lini atarejea uwanjani nadhani hilo sasa ni jukumu la daktari wake aliyefuatana naye huko, atawasiliana na klabu yake kuwaeleza hali halisi jinsi ilivyo na wao ndiyo watakaotoa taarifa rasmi baadaye ya lini atarejea uwanjani," alisema Meneja huyo ambaye aliwahi kuzichezea timu za Kariakoo ya Lindi na 82 Rangers ya Shinyanga.

Hata hivyo habari za ndani zinasema Uongozi wa Simba umeanza mchakato wa kumsaka kipa atakayeziba pengo la Manula hadi pale atakapokuwa fiti. Golikipa wa Vipers ya Uganda Alfred Mudekereza na kipa wa Coastal Union Justin Ndikumana wanatajwa mmoja wapo kumrithi Manula.



Vijana wakicheza mpira wa miguu viwanja vya Jakaya Kikwete jana jioni jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wakongwe wammwagia sifa Mayele

INATOKA UK. 24

wazawa kujifunza kwa Mayele, si kwa ubaya lakini katika kuimarisha uwezo wao, waangalie nini anachokifanya Mayele anapokuwa na asipokuwa na mpira, hata pale timu inapokuwa kwenye wakati mgumu uwanjani Mayele anauwezo wa kushuka chini kuchukua mipira na kukimbia nayo kwenye goli la mpinzani, ni mchezaji wa aina yake kwenye ligi yetu," alisema Kibadeni.

Kibadeni aliendа mbali na kusema hata kwenye kituo chake cha kuzalisha na kukuza vipaji huwa anawafundisha vijana wake wanaocheza nafasi ya ushambuliaji kucheza kama Mayele, muda wote kuwa makini, kusoma mchezo, kumtazama kipa yuko wapi kabla hata pasi au mpira haujafika na kupenda kukaa kwenye maeneo rahisi ya kufunga na si kujikaba.

"Nina kituo changu nafundisha, nawafundisha kucheza kama Mayele na kwa sababu wao wanabahatika kuona video zake, basi inakuwa rahisi, lakini baada ya hapo wanatakiwa kucheza kwa kujitolea, kujituma na kupambana,"alisema Kibadeni.

Naye beki wa zamani wa Simba na Taifa Stars, Amri Said 'Stam' ambaye kwa sasa anafundisha KVZ ya Zanzibar, naye alimfananisha pia Mayele na Mogella kutokana na aina yake ya uchezaji.

Alisema mastraika wanatofautiana aina ya uchezaji, huku akisema walikuwapo kama kina Madaraka Selemani 'Mzee na Kiminyio', Edward Chumila, Makumbi Juma, Malota Soma, ambao aina yao kwa sababu wana nguvu wanaweza kuchukua mpira na kupambana na mabeki huku wakishambulia, lakini Mayele anafanana na Mogella kwa kuwa na uwezo wa kukaa kwenye nafasi na kuweza kuzitumia.

"Mayele ni straika mzuri sana cha kusikitisha kwa sasa Watanzania hatuna aina hii ya mchezaji kwa sasa, inabidi tuwasake huko chini, wachezaji wenye maamuzi ya haraka, kukaa kwenye eneo sahihi na kufanya kitu kwa wakati, haya alikuwa anafanya Mogella na mwingine naweza kusema ni Mohamed Hussein 'Mmachinga'", alisema Amri.

Mayele amekuwa gumzo kwa sasa ndani na nje ya Tanzania kutokana na ubora wake na aina ya mabao yake anayofunga akiwa ameshapachika mabao 16 kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara na mabao saba kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

Aidha, kikosi cha Yanga kinaondoka nchini leo kwa ndege ya serikali kuelekea Algeria kwa ajili ya mchezo wao wa marudiano wa fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya USM Algers.

Yanga inaondoka na baadhi ya mashabiki waliochaguliwa kwenda kuipa nguvu timu hiyo kwenye mchezo wanaohitaji ushindi wa angalau wa mabao 2-0 ili kuweza kutwaa ubingwa wa michuano hiyo.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Idara ya Habari wa klabu hiyo, Ally Kamwe, uongozi wa Yanga umechagua baadhi ya mashabiki watakaowawakilisha wengine kushangilia timu hiyo jijini Algers.

"Yanga inafahamu wanachama na mashabiki wake, tayari utaratibu umeshafanywa na kuteua baadhi ya mashabiki ambao watawawakilisha wengine watakaobaki hapa nyumbani, tusingeweza kuondoka na mashabiki wote, mashabiki na wananchi watuelewe kwenye hili, ndege inachukua mashabiki 260 tu," alisema Kamwe.

Kwenye mchezo wa kwanza uliochezwa Jumapili iliyopita, Yanga ikiwa kwenye uwanja wa nyumbani ilikubali kipigo cha mabao 2-1 hivyo wana kazi ya kutafuta ushindi wa idadi ya mabao kuanzia 2-0 kuweza kutangazwa kuwa mabingwa wa michuano hiyo. Mchezo huo wa keshokutwa utaanza saa 4:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki.

# Gofu wanawake kufanyika Agosti Dar

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya wazi kwa Wanawake ya mchezo wa gofu 'Dar Gymkhana Ladies Golf Open' yamepangwa kufanyika kwenye viwanja vya Gymkhana Agosti 26 na 27.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Mratibu wa mashindano wa Chama cha Gofu cha Wanawake Tanzania (TLGU) ambaye ni nahodha wa timu ya wanawake ya Lugalo, Hawa Wanyeche, alisema lengo la mashindano hayo ni mbali na kuwaweka wanawake pamoja ili kukuza viwango vyao pia watayatumia kupata wachezaji watakaoiwakilisha nchi kwa mashindano ya Gofu ya Afrika Mashariki na Kati yatakayofanyika Rwanda baadaye mwaka huu.

"Lengo la mashindano haya ni kuwaweka wanawake pamoja ili kukuza viwango vyao vile vile tutapata wachezaji watakaokwenda nchini Rwanda kushiriki mashindano ya Afrika Mashariki na Kati katika mashindano haya ya Afrika Mashariki kama TLGU tumepania kufanya vizuri na ndio maana tunatumia mashindano ya ndani kupata wachezaji," alisema Wanyeche.

# Simba yatakiwa kuwatafutia watu Kapombe, Zimbwe

INATOKA UK. 24

sasa wanatakiwa kufanya mabadiliko makubwa kwa kila nafasi huku akitaka wachezaji watakaosajili wawe na uwezo zaidi.

"Robertinho ni kocha mzuri na viongozi wahakikishe wanafanikiwa kumbakiza mwalimu huyo na usajili watakaofanya lazima wafanye maamuzi magumu kwa kuondoa wachezaji ambao hawana msaada na timu na kusajili nyota ambao wana viwango bora, wanatakiwa kuanza kuleta mchezaji ambaye anaweza kumpa changamoto yule anayeanza katika kikosi, lazima wasajiliwe wachezaji watakaowezesha Simba kutoka hapa ilipo na kusogea mbele zaidi,"alisema Kibadeni.

Aliongeza kuwa Simba inacheza michuano mikubwa ya Super League ambayo inashirikisha timu nane bora, wanatakiwa kufanya usajili wenye wachezaji bora ambao watakuwa na hadhi ya kucheza michuano hiyo mikubwa na kufikisha timu hiyo kwenye malengo yao.

Michezo

Alhamisi Juni 1, 2023

Nipashe



## Martial kuikosa fainali ya FA

UKURASA 21



Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Simba, Imani Kajula (wa pili kulia), akiwa pamoja Mkuu wa Programu ya Soka la Vijana wa klabu hiyo, Patrick Rweyemamu na Kocha wa Vijana, Seleman Matoka (wa pili kushoto), baada ya kutangazwa kushika nafasi hizo jana. **PICHA: BINZUBEIRY**

# WAKONGWE WAMMWAGIA SIFA MAYELE YANGA IKIENDA ALGERIA

●●●Wamfananisha na nyota wa zamani Taifa Stars, wataka wazawa kujifunza kwake, Uongozi wateua mashabiki waondoka nao...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WAKATI kikosi cha Yanga kikitarajiwa kuondoka leo kuelekea Algeria kwa ajili ya mchezo wao wa marudiano dhidi ya USM Alger Juni 3, wachezaji wa zamani hapa nchini wamemfananisha mshambuliaji wa timu hiyo na nyota wa zamani wa timu ya taifa 'Taifa Stars' Zamoyoni Mogella na kuwataka washambuliaji wa sasa kumuiga nyota huyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Mshambuliaji na Kocha wa zamani wa klabu ya Simba, Abdallah Kibadeni, amesema hakuna tofauti kati ya Mayele na Mogella kwani ni wachezaji hatari muda wote wanapokuwa kwenye eneo la hatari.

"Mayele ni mshambuliaji mzuri na aliyekamilika, anayeijua vizuri kazi yake, hivi mnavyomwona alivyo ni kama zamani alivyokuwa Mogella, pamoja na kwamba kulikuwa na washambuliaji wazuri, lakini aina au staili ya uchezaji inafanana, Mogella anaweza kukabwa muda wote, lakini nusu nafasi tu ukimwachia anakumaliza na alikuwa na uwezo wa kufunga mabao kwenye maeneo yote, ndani ya box, mbali na goli, pembeni kulia au kushoto, kifupi akiwa na mpira tu alikuwa ni hatari, hii tunaiona sasa kwa Mayele, ni mshambuliaji aliyekamilika kwenye kila idara," alisema Kibadeni.

Alisema mafanikio ya sasa ya Yanga yanachagizwa na ubora wa mshambuliaji huyo ambaye mpaka sasa ni kinara wa ufungaji katika Ligi Kuu na michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

"Kuna umuhimu kwa wachezaji wetu

INAENDELEA UK. 23

## Simba yatakiwa kuwatafutia watu Kapombe, Zimbwe

**Na Saada Akida**

HUKU uongozi wa klabu ya Simba ukiwa kwenye mchakato wa kukiboresha kikosi chao kwa ajili ya msimu ujao, mchezaji na kocha wa zamani wa klabu hiyo, Abdallah Kibadeni ameutaka uongozi huo kutofanya makosa katika usajili huku akishauri kutafutwa wachezaji wenye ubora mkubwa kwa ajili ya nafasi ya mabeki wazoefu Shomari Kapombe na Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr'.

Kibadeni amesema ameangalia kikosi cha Simba kinahitaji kufanya maboresho makubwa na kuwataka viongozi kusajali wachezaji ambao amewapendekeza kocha wa timu hiyo, Roberto Oliviera (Robertinho).

Akizungumza na Nipashe





jana, Kibadeni alisema amemfuatilia Robertinho kipindi kifupi na kuona mabadiliko ya kikosi cha Simba na anaimani viongozi wakimwachia jukumu la kufanya usajili kwa kuleta wachezaji anaowahitaji timu hiyo itafanya vizuri msimu ujao.

Alisema kulingana na kikosi cha Simba kwa

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >